

**KULINGANISHA MIKO NA TASFIDA YA WASWAHILI**

**(WAJOMVU) NA WARABAI**

**MUNGA DUNCAN SHONGWE**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA  
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI KATIKA  
CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**NOVEMBA 2015**

## **UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na hajatolewa katika chuo kikuu chochote kingine kile kwa minajili ya kuitosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

Sahihi ..... Tarehe .....

**MUNGA DUNCAN SHONGWE**

C50/75491/2012

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini ya wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu Cha Nairobi.

**PROF.MOHAMMED ABDULAZIZ**

Sahihi ..... Tarehe .....

**PROF. KINEENE WA MUTISO**

Sahihi ..... Tarehe .....

## **TABARUKU**

Natabaruku kwa mama yangu mzazi, Sarah Mnyazi Munga, aliyenitia matumaini ya kuhitimu shahada ya Uzamili. Namtabarukia pia marehemu baba yangu Ezekiel Munga Mwamkale, aliyechangia kufaulu kwangu katika masomo yangu na aliyekuwa akiniambia kwamba nisome kwa bidii hadi nifikie kilele cha masomo yangu.

## SHUKRANI

Tasnifu hii imewezeshwa na ukarimu, juhudi na hisani za watu mbalimbali, nitawataja watu wachache tu kwani ni wengi waliochangia utafiti huu. Natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Profesa Mohammed Abdulaziz na Profesa Kineene wa Mutiso kwa uongozi wao, kuanzia mwanzo hadi tamati ya tasnifu hii. Waliniongoza na kunifungua macho katika ulimwengu wa usomi kwa njia za kipekee kabisa. Ningependa kuwashukuru pia wahadhiri wengine ambao walioniandaa kufikia kuweza kukabili kazi hii ya kitaalamu kiasi hiki. Hawa ni Profesa John Hamu Habwe, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt Zaja Omboga, Dkt. Iribi Mwangi, Dkt. Mwenda Mbatia, Dkt. Amir Swalehe, Bw. Basilio Mungania na Dkt Mbuthia. Mwalimu wa shule ya upili ya Dr Krapf ,Bwana Daniel Gonzi kwa msada wake wa kutowa makosa alipoipitia kazi hii.

Shukrani zingine ziende kwa wanafunzi wenzangu tuliosoma pamoja. Hawa ni Samuel Mwakuyua, aliyenitia shime kila kukicha, Nashon Nyangeri, Vincent Otieno, Sister S. Waweru, DoriceKachipela, Jael, Regina Gitau, Julius Mwangi, Mariam Ngome, Furaha M'mbetsa, Scolastica Waweru na mwisho ni Ruth M. Binyanya, aliyekuwa mwakilishi wetu wa darasa.

Pia ningependa nimtolee mke wangu mpendwa Christine Shongwe shukrani za kipekee kwa subira, uvumilivu, uwajibikaji na kwa kunipa moyo mambo yalipokuwa ni magumu. Zingine ziende kwa watoto wangu, Jonathan Mbaji Shongwe, Veronica Msaveki, Douglas Namai Shongwe, Ezekiel Munga Shongwe, na William Kamoti Shongwe (Mbunge).

Sitawasahu wazazi wangu wapendwa, Ezekiel Munga na Sarah Munga kwa malezi bora ya hali na mali tangu nilipokuwa mtoto mdogo. Hatimaye, namshukuru Mungu kwa kuwa mwamba na mwangaza wangu wakati wa shida na wakati wowote mambo yaliponijia mema na mabaya kwani ndiye aliyekuwa tegemeo langu.

## **IKISIRI**

Warabai ni mojawapo wa makabila yanayoungana pamoja kuunda kundi moja lijulikanalo kama Mijikenda. Baadhi ya makabila yanayounda kundi la Mijikenda ni pamoja na Waribe, Wagirlama ambao ni wengi kuliko makabila mengine ambayo ni pamoja na Wakauma, Wajibana, Wachonyi, Wakambe na Warabai wanaopatikana katika kaunti ya Kilifi na kunayo makundi yanayopatikana katika kaunti ya Kwale. Nao ni Wadigo na Waduruma. Wote wakiwa makabila tisa wakiitwa Wamijikenda, ni Wabantu ambao chimbuko lao ni msitu wa Kongo ulioko Afrika ya Kati. Walitoka Kongo kwa sababu ya kutafuta makaazi mapya baada ya idadi ya wabantu walioishi huko kuongezeka. Kila kundi la wabantu walipotoka Kongo walishika njia yao. Hii ilipelekea kufika sehemu wanamoishi sasa.

Hapa walikuja kuwa na ujirani na Waswahili ambao ni wabantu pia. Waswahili kama vile Wamijikenda wana makabila kumi na mawili. Makabila haya kumi na mawili ya Waswahili ndiyo yaliyokuwa na idadi kubwa ya wakaazi wa kisiwa cha Mombasa. Kulikuwa namuunganowa makabila matatu ya Wakilindini, Wachangamwe, Watangana (miji mitatu). Makabila ya Mvita yaliundwa na Wamvita, Wakilifi, Wamtwapa, Wapate, Washaka, Wagunya, Wakatwa, Wafaza, na Wajomvu. Majina ya makabila haya yatujulisha kwamba takribani saba yao, tukitenga Wa-mvita na Wajomvu yalitoka makao ya zamani ya Waswahili kaskazini mwa Mombasa. Wajomvu wanao julikana kwa ujuzi wao wa kutengeneza vyungu Pwani. Bado wanaishi katika makaazi yao yapatikanayo kando kando ya mkondo wa Bahari Hindi Mombasa ui twao Maungunja na Jomvu Kuu.

Wanaongea lafudhi iliyo tofauti na ya Kiswahili cha Ki-mvita. Na yale makabila matatu yaliundwa na Wa-kilindini, Wa-changamwe na Wa-tangana.

Kando na makabila kumi na mawili ya Waswahili walikuwa na urafiki na Wamijikenda wa Nyika. Wamijikenda walichangia sana katika siasa na vita vyta Mombasa. Kwa vile walikuwa wajuzi wa kutumia upinde na mishale walikuwa jeshi muhimu la Mombasa katika vita na Wapate na Waomani. Hii ilikuwa sababu mojawapo ya ushirikiano baina ya Waswahili na Wamijikenda, pamoja na kuoleana mabinti zao. Hii ilisababisha Wanyika (Wamijikenda) kuwaita Waswahili 'adzomba' kumaanisha wajomba na wapwa. Wamijikenda waliuzia watu wa Mombasa bidhaa nyingi kama vile 'gumcopal'. Ushirikiano baina ya Waswahili na Wamijikenda ulifanikishwa na wazee wamiji kama vile Tamimu aliyejikuwa mmoja wa yale makabila matatu ya Waswahili.

Kwa hivyo tunaona makundi haya mawili ya Wamijikenda na Waswahili waliokuwa na ushirikiano mwafaka ndio sababu tukatafiti juu ya miiko na tasfida yao na tukalinganisha Tulijikita katika Warabai kwa niaba ya Wamijikenda na Wajomvu kwa niaba ya Waswahili kwani hawa wameishi kwa ujirani wa tokea kale.

Utafiti huu unahu unahusu uwasilishaji na majukumu ya Miiko na Tasfida ya Warabai na Waswahili. Kazi hii imegawanyika katika sura nne. Katika sura ya kwanza tumeangazia maswala muhimu ya utafiti wetu. Tumeelezea swala la utafiti, madhumuni na nadharia tete zilizotuongoza. Aidha, sababu za utafiti na upeo na mipaka zimeelezwa. Msingi wa nadharia wa utafiti umefafanuliwa, na yaliyoandikwa kuhusu mada yalijadiliwa.

Mwisho, mbinu za utafiti zimebainishwa na uwasilishaji wa data umefanywa. Katika sura ya pili, tumeshughulikia fasili na asili ya Miiko na Tasfida ya Warabai na Waswahili. Aidha, katika sura ya tatu, tumezungumzia misamiati ya Miiko na Tasfida ya Warabaina vilevile Waswahili. Pia tumeshughulikia mikakati ya matumizi ya Miiko na Tasfida. Pia tumeshughulikia majukumu yanayojitokeza katika Miiko na Tasfida ya Warabai na Waswahili. Sura ya nne, ambayo ndio mwisho, tumejikita katika matokeo ya utafiti, changamoto tulizokumbana nazo. Pia tumetoa mapendekezo ya utafiti wa baadaye kuhusu mada hii. Msingi wa nadharia uliotumiwa ni wa nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987).

Lengo la utafiti huu ni kuchunguza na kufafanua miiko na tasfida itumiwayo sana na Warabai na vile vile Waswahili, ili kuasisi taarifa na maana za tasfida na miiko ya lugha ya Kirabai na Waswahili, kuchunguza majukumu ya Miiko na Tasfida zitumiwazo na Warabai na Waswahili. Data ya utafiti ilikusanya kutoka kwa watafitiwa ishirini wake kwa waume Warabai wa kutoka kata ndogo ya Rabai, wilaya ya Rabai na Gatuzi la Kilifi na vilevile Waswahili wa Jomvu Gatuzi la Mombasa. Hii ni kwa sababu kwamba mtafiti ni mzungumzaji wa lugha ya Kirabai izungumzwayo Gatuzi la Kilifi. Pia kuhoji watafitiwa Wajomvu. Matokeo yaonyesha kwamba ili kuepuka kufedhehesha, Warabai na Waswahili hujaribu kutafuta maneno mbadala ambayo huficha aibu kuliko kutumia maneno ya miiko. Hivyo basi hutumia tasfida kuepuka yale maneno ya aibu na yawezayo kuleta aibu kwa mzungumzaji wa Kirabai.

## YALIYOMO

<b>UNGAMO .....</b>	<b>ii</b>
<b>TABARUKU .....</b>	<b>iii</b>
<b>SHUKURANI .....</b>	<b>iv</b>
<b>IKISIRI .....</b>	<b>v</b>
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
1.1 Utangulizi .....	1
1.2 Tatizo la Utafiti.....	5
1.3 Madhumuni ya Utafiti.....	7
1.4 Nadharia Tete .....	7
1.5 Sababu Za Kuchagua Mada.....	7
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	8
1.7 Msingi wa Kinadharia.....	9
1.8 Yaliyoandikwa Kuhusiana na Mada.....	17
1.9 Mbinu Ya Utafiti .....	26
1.10 Hitimisho.....	28
<b>SURA YA PILI: MIIKO NA TASFIDA.....</b>	<b>29</b>
2.1 Utangulizi .....	29
2.2 Fasili ya Mwiko .....	29
2.2.1 Uhusiano baina ya Miiko na Tasfida .....	30
2.2.2 Uhusiano baina ya Mila za Kirabai na Kiswahili na Miiko Kilugha .....	33
2.3 Asili ya Miiko na Tasfida Katika Jamii ya Warabaina Waswahili .....	35
2.3.1 Kijamii na Hali ya Matumizi ya Kawaida ya Lugha .....	35
2.3.2 Kanuni za Matumizi ya Miiko.....	37
2.3.3 Kuombwa kutoka lugha za Kigeni.....	39
2.3.4 Umuhimu wa miiko na Tasfida .....	40
2.4 Mhtasari na hitimisho la sura ya pili.....	40

<b>SURA YA TATU: UWASILISHAJI MIKO NA TASFIDA YA WARABABAI NA WASWAHILI .....</b>	<b>42</b>
3.1 Utangulizi .....	42
3.2 Uwasilishaji wa Data juu ya Miiko na Tasfida. ....	42
3.2.1 Msamiati wa Ngono .....	43
3.2.2 Msamiati wa mimba na kuzaa .....	46
3.2.3 Msamiati wa kubaka .....	47
3.2.4 Hedhi .....	49
3.2.5. Kunya .....	52
3.2.6. Kukojoa .....	53
3.2.7 Mwiko wa Kifo .....	55
3.2.8 Miiko ya Magonjwa –Ukimwi.....	60
3.2.9 Ukimwi.....	61
3.2.10 Miiko na Tasfida ya Kubalehe ya Warabai .....	64
3.3 Miiko ya Vyakulavisiviyoliwa na Warabai .....	66
3.3.1 Miiko na Tasfida ya Wanyama Wasioliwa .....	67
3.3.2 Miiko na Tasfida ya Ndoa .....	68
3.4 Hitimisho.....	71
<b>SURA YA NNE: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>73</b>
4.1 Utangulizi .....	73
4.2 Muhtasari na Hitimisho.....	73
4.3 Mapendekkekezo .....	76
4.4 Hitimisho .....	76
<b>MAREJELEO.....</b>	<b>78</b>
<b>VIAMBATANISHO</b>	

## SURA YA KWANZA

### 1.1 Utangulizi

Utafiti huu unachanganua na kufafanua uhusiano uliopo baina ya maana na fasili ya Tasfida na vile vile maneno ya Miiko katika miktadha inapotumiwa na wazungumzaji wa Kirabai kama lugha ya kwanza na vilevile Waswahili wa Jomvu. Tasfida imeelezwa katika *Longman Dictionary ya ufunzaji lugha na isimu 2010, 3<sup>rd</sup> edition la Richard J. and R. Schmidt* kama “matumizi ya neno ambalo laonekana kama lisilo kera zaidi kuliko maneno mengine”. Katika Penguin Dictionary of Literacy terms (1976) tasfida imelezwa kuwa “neno mbadala la lile lenye kukera”.

Leech and Brown (1995-269), wanaeleza kwamba tasfida ni neno ama msemo ambao watu hutumia badala ya neno ambalo halifai kutumiwa na mzungumzaji kwa hadhira au wasikilizaji. Msemo unapokuwa tasfida, maana yake ya awali hupotea kwa sababu tasfida hutumiwa kuficha mambo yasiyopendeza kwa mzungumzaji na vile vile msikilizaji. Tasfida hutumiwa kufanya yanayozungumziwa kupendeza kwa wasikilizaji. Yahuksiana na hali ya jumla za matumizi ya lugha katika mawasiliano. Tamaduni zote hutumia tasfida zinapozungumzia mambo ambayo yana matusi au yanayokera kwa upole.

Kwa mfano, maneno ya tasfida yatumiwayo kuwasilisha hali au mambo kama vile magonjwa, kifo, ngono, kubaleghe, ndoa, vyakula visivyoliwa na wanyama wasioliwa kwenda haja kubwa na ndogo. Kwa hivyo, tasfida hutumiwa kuelezea maneno ya miiko kwa upole ili kuepuka kutumia maneno machafu au ya matusi. Misemo ya miiko husimamia marufuku ya matumizi ya maneno yatokanayo na mila na desturi ya watumizi

wa lugha. Allan and Burridge (2006), wanasema kwamba miiko ni mambo yanayozungumzia tabia zinazoathiri mambo ya kila siku na wanasema watu kawaida huepuka mambo ya miiko isipokuwa wanapotaka kutumia maneno ya miiko kimakusudi wakitaka kuwasilisha jambo nyeti.

Evan n.w. (2000:2), anakubaliana na kusema kwamba miiko hudhibiti hali yetu ya maisha ya kila siku na huweka mipaka ni nini cha kukubalika au kutokubalika, lililo sawa na lisilo sawa katika jamii.Kwa hivyo miiko ya isimu ni neno lolote au usemi au mada ambayo itajwapo hadharani husababisha fedheha na aibu ambayo huathiri hisia au imani ya msikilizaji.

Maneno ya miiko huepukwa katika hali fulani ya muktadha wa mzungumzaji na wasikilizaji katika mchanganyiko wa uhusiano au uhusiano wa upole mbele ya watu.Msamiati amba ni mwiko huonekana kutofaa katika miktadha fulani. Kitu chochote kilicho mwiko hutokana na mila na hakuna kitu asili katika lugha husika na haswa katika lugha ya Kirabai. Miiko hurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi kingine. Nyingine hupoteza umaarufu miaka inapoenda na huachiliwa mbali vile jamii inavyobadili na mingine kujitokeza kwa mujibu wa mila na mabadiliko ya kijamii na hali ya usasa. Miiko nyingine hutokea kwa uhusiano wa migusano ya kikabila.Miiko hubebwa na lugha za mtumizi lugha.

Hapa tunalinganisha miiko na tasfida ya Warabai na Waswahili lahaja na Kijomvu. Wajomvu ni Waswahili amba wanazungumza lahaja ya Kiswahili iitwayo Kijomvu.

Asili ya Kijomvu ni Warabuni pahali paitwapo Al-Jofi. Walitoka Warabuni kwa sababu ya kukimbia kulipizwa kisasi baaada ya kukosea watu wengine huko Warabuni. Walipotoka Warabuni walitorokea Shungwaya wakiwa kundi moja kubwa la Wajomvu. Hapo Shungwaya pia walikosana na kuteta, iliyopelekea wagawanyike wengine waende nchi ya Ethiopia na nchi nyingine. Lakini wengine waliotawanyika Shungwaya walikuja mkoani Pwani. Walikuwa wazawa wa Kiislamu. Walikuja Kenya kabla ya Wareno na Waarabu.

Nyimbo zao za kuomboleza mtu anapokufa walikuwa na ngoma yao waliyoita goma au tutu walilolipiga mtu mzima aagapo dunia. Tutu lilipigwa kujulisha mtu mzima amekufa pia goma la ‘tutu’ lilipigwa kujulisha watu kwamba harusi iko karibu. Walifanya maulidi au kuimba nyimbo za maulidi maiti akiwa anaoshwa. Mtu afapo wanawake waliomboleza kwa kuimba nyimbo za dua- kama vile wimbo “Aila ilala Muhamadi; Allah sululah.” Pia husoma maulidi mtu afapo. Mila zao kwa wakati huu ni uislamu. Zamani mtoto kabla hajatahiriwa wangeenda pangani kutafuta nguvu lakini siku hizi wanafuata dini ya Kiislamu. Walipotoka Shungwaya walikuja mpaka Gede, Takaungu na Mkomani baada ya kutoka Mkomani walienda hadi Mji wa kale. Baadaye walihama kutoka Mjiwakale wakaja hadi Jomvu ya Kwa Shee ndugu ya Shekhe wa Mvita, wakakaa hapo baadaye wakaja Jomvu Kuu.

Jomvu kuu ilitokana na kwamba kundi la Wajomvu waliohamia hapa lilikuwa kundi kubwa- kuu. Mzee mmoja wa Kijomvu aitwaye Mwinyi Ngutu alienda Zanzibar kutafuta usaidizi wa kumfukuza Mreno na baadaye Mwarabu akachukuwa utawala wa Mombasa.

Wajomvu waliteta wenyewe kwa wenyewe iliyosababisha watengane wengine waende Mwandoni ambako pia waliteta wenyewe kwa wenyewe na kupelekea kutawanyika na kwenda Maunguja.

Idadi yao ni takribani watu elfu kumi hivi. Huoana waislamu kwa waislamu au kama bwana si muislamu basi ilimbidi aslimu. Kubadili dini na kuwa muislamu huitwa kutanasari, ili aweze kuoa muislamu. Zamani watu walikuwa wakioana mwezi wa kabla ya Ramadhani na baada ya Ramadhani. Wajomvu wanapatikana sehemu kama vile Kaloleni, Rabai, Kinango na Ukambani. Kazi yao kuu ni uvuvi kwa wanaume na uumbaji vyungu kwa wanawake. Vile vile hufanya biashara ya duka na kulima.

Jina Waswahili lilitokana na neno la Kiarabu “Saheli” limaanishalo kusini kwa lugha ya Kiswahili sanifu. Warabai ni mojawapo wa makabila yanayoungana pamoja kuunda kundi moja lijulikanalo kama Mijikenda. Baadhi ya makabila yanayounda kundi la Mijikenda ni pamoja na Waribe, Wagirlama ambao ni wengi kuliko makabila mengine ambayo ni pamoja na Wakauma, Wajibana, Wachonyi, Wakambe na Warabai wanaopatikana katika kaunti ya Kilifi na kunayo makundi yanayopatikana katika kaunti ya Kwale. Nao ni Wadigo na Waduruma. Wote wakiwa makabila tisa wakiitwa Wamijikenda, ni Wabantu ambao chimbuko lao ni msitu wa Kongo ulioko Afrika ya Kati. Walitoka Kongo kwa sababu ya kutafuta makaazi mapya baada ya idadi ya Wabantu walioishi huko kuongezeka. Kila kundi la wabantu walipotoka Kongo walishika njia yao. Hii ilipelekea kufika sehemu wanamoishi sasa.

Hapa walikuja kuwa na ujirani na Waswahili ambao ni wabantu pia. Waswahili kama vile Wamijikenda wana makabila kumi na mawili. Makabila haya kumi na mawili ya Waswahili ndiyo yaliyokuwa na idadi kubwa ya wakaazi wa kisiwa cha Mombasa. Hii ilimaanisha watu wapatikanao kusini mwa Uwaarabuni. Kwa mfano, miiko hukataza kutaja sehemu nyeti za mwili kwenye hadhara na vile vile matendo ya kimwili hadharani lakini kwenye maombolezi na matanga ya Warabai huwa zatajwa kuitia nyimbo za maombolezi kama vile wimbo wa Warabai wa maombolezi.

“*Chimbwambwa bolo ni dzogofya*”, “bolo” in uume.

Wimbo huu huimbwa kwenye halaiki ya waombolezaji bila hofu yoyote kilugha. Hutumika kulingana na miktadha na jinsia ambazo pia huwa zimejengwa na utamaduni, kuna mambo ambayo watu wa tajriba tofauti huwa hawawezi kuyasema bali wenyе tajiriba moja huyatumia. Katika Waswahili hususani Wajomvu ambao ni Waislamu huimba nyimbo za dua za kiislamu. Nyimbo hizi huimbwa na wanawake kwenye nyumba iliyo na maiti akiwa anaoshwa. Mfano wa wimbo za Waislamu ni kama vile, “Aila ilala Muhamadi alasulula” Tasfida ni matumizi ya maneno ya ustaarabu kuelezea miiko yasiyokera mzungumzaji wala msikilzaji. Katika utafiti wetu tumechunguza kama madai haya yana ukweli katika lugha ya Kirabai na vilevile Kiswahili.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu ulihusu mwingiliano baina ya lugha na utamaduni. Unajikita katiaka jambo liitwalo miiko na tasfida, mwiko humaanisha jambo lolote ambalo limekatazwa katika

jamiilugha husika. Semi za tasfida hutumika kuepuka kunena maneno fulani yaliyokatazwa au kueleza mambo ya matendo ya kimwili kama vile ngono, kunya, kojoa, ugonjwa wa Ukimwi, ndoa, vyakula visivyoliwa na Warabai na Waswahili, wanyama wasioliwa na Warabai na Waswahili, kuzaa na kubaka. Wardhaugh (2002:237), mwiko ni kitu kilichokatazwa katika jamii au tabia ambayo yaaminika kuwadhuru jamii kwa kuleta aibu. Mambo ambayo huwa ni mwiko huwa tofauti tofauti kama vile ngono, kifo, magonjwa, uuaji, uzazi, utoaji mimba, kuingia mwezini, kubalehe, na kubaka.

Trudgill (2000:18), anasema kuwa thamani ya jamii yaweza kuleta athari katika lugha ya jamii wanayozungumza. Hii ni kupitia mambo yanayokatazwa ambayo ni mwiko kutumika katika mazungumzo ya kawaida. Mwiko waweza kuwa mambo ambayo yahusishwa na mambo yaliyokatazwa na dini au mambo ambayo ni kinyume na tabia njema.

Katika lugha, miiko huhusishwa na mambo ambayo hayasemwi ovyo ovyo, na vitendo vya kimwili ambavyo havifanywi hadharani. Hii inamaanisha marufuku ya matumizi ya kawaida ya mambo haya. Tasfida ni matumizi ya maneno ya staha badala ya yale ya mwiko, kwa mfano, “mtu huaga dunia” badala ya kufa. Tasfida ni kusema kitu ambacho chaashiria au thibitisha mambo ambayo yalikuwa yamaanisha kitendo cha kuudhi (Ortony (1993:43). Katika utafiti huu tumelenga kuchunguza maneno ya miiko na maneno mbadala yatumiwayo kama tasfida kwa yale ya miiko. Hii imewiana na utafiti wetu wa miiko na tasfida ya Warabai na kulinganisha na miiko na tasfida ya Waswahili.

### **1.3 Madhumuni ya Utafiti**

Kuchunguza misamiati tofauti tofauti itumiwayo kama tasfida kwa maneno ya miiko. Kuchunguza kuwepo kwa matumizi ya maneno ya miiko na tasfida katika lugha ya Kirabai na na vilevile Kiswahili. Kuchunguza kama tofauti za kijamii kama vile uwana na miaka huathiri mitazamo ya watu kuhusu uchaguzi na matumizi ya tasfida.

### **1.4 Nadharia Tete**

Utafiti umejikita katika nadharia tete zifuatazo:

Je, Warabai hutumia tasfida kwa kiasi gani kuepuka kutumia msamiati wa miiko?

Je, Waswahili hutumia tasfida kwa kiasi gani?

Je, Uchaguzi na ufasiriaji wa tasfida huathiri viwango vya lugha katika jamii kama vile jinsia na umri wa wazungumzaji na wasikilizaji?

Je, Miiko na tasfida ya Warabai na Waswahili yafanana?

### **1.5 Sababu Za Kuchagua Mada**

Warabai, ambao ndio mada ya utafiti, ni baadhi ya makundi tisa yaundayo kundi liitwalo Mijikenda. Kulingana na Spear (1978), ni wakulima na wafugaji tangu walipokuwa Shungwaya. Mbali na kwamba walikuwa wakulima, walikuwa pia wafanya biashara. Walifanya biashara na Wamijikenda wengine na hata wageni. Ingawaje, watazamiwa kupatikana Wilayani ya Rabai, pia hupatikana maeneo mengine kama vile Mombasa. Sababu yao ya kutumia tasfida ni kuficha mambo ya aibu na yenye kutisha. Hii humuepusha mzungumzaji na masikilizaji kupata aibu.

Lengo la utafiti huu ni kutafiti vile miiko na tasfida hutumika katika lugha ya Kirabai na vile vile Waswahili. Hii pia inakusudiwa kuwawezesha Warabai na Waswahili watakao usoma utafiti huu kabla na baada ya kuchapishwa kutumia tasfida katika lugha ya Kirabai na vilevile Kiswahili kwa mwafaka. Kwa vile utafiti unatumia nadharia ya Upole, utafaidisha yule atakayeonelea kufanya utafiti juu ya tasfida akitumia nadharia zingine. Kulingana namtafiti, hakuna utafiti juu ya miiko na tasfida umefanyiwa katika kulinganisha lugha ya Kirabai na Kiswahili.

Basi sababu maalum ni kwamba ni kuziba pengo lililopo katika uchambuzi wa miiko ya Warabai na ya Waswahili. Sababu nyingine iliyonifanya nichague mada hii ni kutaka kuchangia kimawazo katika fasihi simulizi. Hali hii itawaelimisha watu kutoka jamii nyingine kufahamu utamaduni wa jamii zingine. Kwa sababu maneno ya mwiko hayatumiki kimazoea, ndio sababu tuliona tutafiti juu yake ili yasiweze kupotea katika jamii ya Warabai na Waswahili. Pia, baada ya kutafiti tuyaweke kwenye maandishi ili kufaidi vizazi vijavyo, vile vile tuweze kuchangia katika uandishi na ili kuweza kuyahifadhi katika kanda za sauti.

## **1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Katika utafiti wa kiisimu ya jamii kama huu wa sasa, neno mwiko laashiria marufuku kwa matumizi ya misamiati maalumu. Katika ufanuzi wa miiko na tasfida ni maana mbali ya neno moja (Grady, W et al 1997). Kuna lahaja mbili za Kirabai, Kirabai cha Rabai Mpya na Kirabai cha Kiruruma. Kwa madhumuni ya utafiti wetu, tutazingatia Kirabai cha kata ndogo ya Rabai na kulinganisha na miiko na tasfida ya Waswahili:

Wajomvu wa Gatuzi la Mombasa Tumejikita kwa lahaja moja ya Kirabai na lahaja ya Kijomvu ya Kiswahili. Mtafiti kwa hivyo atatumia uzoefu wake kama mzungumzaji wa lahaja ya Kirabai na kulinganisha Kiswahili. Katika Waswahili tulishughulikia Wajomvu wa Jomvu kuu. Hii ni kwa sababu Wajomvu wametapaka katika sehemu nyingi Pwani, wanapatikana sehemu kama vile Maunguja, Kaloleni, Rabai na hata Kinango, Kwale. Vilevile Jomvu kuu imepakana na Rabai ambayo pia ni mojawapo ya kiini cha utafiti wetu.

Kando na hayo, eneo la Rabai ni pana kufanya utafiti mada hii ya miiko na tasfida. Kwa kusudi la utafiti wetu, tutajikita katika magonjwa-UKIMWI, kubalehe, kifo, kubaka, ngono, ndoa, wanyama wasioliwa, vyakulavisivyoliwa, hedhi, mimba na kuzaa. Zaidi ya hayo, kuna tabia ya wazungumzaji au watu ya kutumia tasfida ili kufanya mambo yanayokera kuvumilika. Hii hulenga kuficha hisia zao au malengo yao yasiwe wazi. Utafiti umetumia mkakati huu katika utafiti wa miiko na tasfida ya lugha ya Warabai. Lengo la kutumia mipaka hii ni kutuwezesha kuwa na data ili kufanya kazi kando na kuweka asili ya miiko na tasfida katika lugha ya Kirabai na Kiswahili.

### **1.7 Msingi wa Kinadharia**

Nadharia nyingi zimetumiwa katika utafiti juu ya miiko na tasfida. Baadhi ya nadhara hizi ni pamoja na ile ya Halliday's ya Misemo jamii (1978), ile ya Austin ya matendo ya matamshi (2002), na Robin Lackoff ya upole au nadharia ya uso (1973). Nadharia hii ya Lackoff iliendelezwa na Brown na Levinson (1987).


Utafiti wetu wa sasa utatumia nadharia ya baadaye ya Brown na Levinson (1987).

Kulingana na Lackoff, watu wanapoongea huzingatia kaida za kitamaduni, kuonyesha kwamba ni sehemu ya wazungumzaji lugha husika.

Kwa hivyo watu watajibidisha:

Kuwa wazi

Kuwa wapole



Ilichukuliwa na kurekebishwa kutoka <http://www.scribd.com/doc/4981649/> mikakati ya nadharia ya upole. Katika mazungumzo kila wakati wazungumzaji huwa wanajaribu kutimiza mahitaji haya. Lakini, kama sheria hizi zahitilafiana, upole huchukua nafasi kwa sababu ni muhimu sana katika mawasiliano kuepuka fedheha kuliko uwazi. Hii ni kwa sababu katika mazungumzo ya kawaida, uwasilishaji wa maoni si jambo la msingi kuliko kudumisha uhusiano. Kanuni ya uwazi ina vijikanuni vinne, navyo ni kiasi, ukweli, uhusiano na namna. Kanuni ya kiasi, hupima idadi ya mambo yanayo

zungumziwa hivi kwamba inamhitaji mzungumzaji asizidishe wala kupunguza aliyoamua kuyasema ili aweze kuwasiliana na kueleweka vyema. Yaani habari ya mzungumzaji iwe kamilifu.

Kanuni ya ukweli nayo inamtaka msemaji asiseme mambo ambayo hana hakika nayo wala ushahidi nayo ili asidanganye. Msemaji aseme yale aliyo na ushahidi nayo na anayajua ni ya ukweli. Ilhali katika kijikanuni cha uhusiano chasema mzungumzaji asitoke nje ya mada inayoendelea wakati huo.

Kile kijikanuni cha namna chasema mzungumzaji atakikana aseme mambo kwa uwazi yasiwe na utata ili mawasiliano yadhihirike. Aseme mambo kwa utaratibu wenye mantiki. Nadharia ya upole ya Lackoff ina kanuni tatu, ambazo ni;

Usishurutishe

Peana nafasi ya changizo au maoni

Uwe tayari kukubali

Vijisheria hivi ingawaje hutoa habari nyingi, ni vigumu kuelewa kwa sababu lugha ina hali nyingi za kuzielezea. Kwa mfano, kusema chakula chapakuliwa “ni upole kuliko kuuliza” ungetaka kula? Katika sentensi ya kwanza inafuata sheria (1) ya hapo juu kwani inaepuka kuingilia matakwa ya msikilizaji na kwa hivyo unapeana nafasi kwa msikilizaji. Katika sehemu (11), wazungumzaji hupeana wasikilizaji nafasi ya kufikiria jibu la kutoa bila kushurutishwa. Sentensi mbili zifuatazo za Lackkoff (*Ibid*) zasaidia kufafanua sheria hii zaidi.


Nafikiria ni wakati wa kuondoka.

Ni wakati wa kuenda, au la?

Sheria (III) ya Lachoff ambayo inamwomba mzungumzaji amfurahishe msikilizaji ndiyo njia mwafaka iletayo maana. Sheria hii inamaaanisha wanaowasiliana washirikiane na kutathmini mazungmzo kulingana na malengo yao. Wakiongozwa na Lackoff juu ya upole, Brown na Levinson (1987), wanasema kwamba kila tabia ya upole imejikita katika dhana kwamba ushirikiano katika jamii wahitaji kupunguza mtafaruku katika jamii.

Katika nadharia ya Brown na Levinson's (1987), neno Upole lahusika na Uso ambao wanasema ni jambo la kibinagsi au katika jamii. Wazo hili la neno uso lahusisha aina nyingi za matamanio au tamanio la Uso ambalo watu wote wanalo na ambalo watu wote wajua wanalo. Matamanio haya ya uso yako aina mbili kimsingi;

1. Uso chanya- Hii ni hali ya mtu kutaka kutambulika.
2. Uso hasi- Hii ni hali ya mtu kutotaka kuingiliwa mambo yake.



Brown na Levinson (1987), wanasema ingawaje mahitaji ni ya kijumla, yanafungamana na utamaduni. Ni mambo gani hutishia uso? Mtu aina gani ana haki za kipekee kwa mahitaji ya kulindwa uso?


Ni mitindo gani ya maisha katika mambo ya hisani na uhusiano wa kijamii hutambulika vyema (Bonvillain 1997:118). Brown na Levinson wanapambanua mikakati ya tabia ya upole kwa kutofautisha mahitaji ya uso. Upole Chanya: Hapa mhusika hupenda kutambuliwa na kuhusishwa kwenye jambo. Upole chanya hudhihirisha ushirikiano na urafiki kwa ujumula.

Uso Hasi- Hii ni hali ambapo msikilizaji hapendi kuingiliwa mambo yake. Hapa mzungumzaji humtambua msikilizaji na uhuru wake wa uamuzi wa mambo. Mikakati ya upole hasi huonyesha hali ya mzungumzaji ya kujizuia na kuepuka kumuingilia msikilizaji. Upole wa nje- ya rekodi –hii yahusiana na hali ya kutumia mikakati isiyo ya wazi ambayo huepuka kushurutisha mambo kwa msikilizaji. Wazungumzaji huteua baadhi ya mitindo hii na vibadala vya kiisimu, kwa kutegemea uhusiano wao na hadhira katika mikitadha ya kijamii kuhusiana na ujumbe.

Kulingana na Brown na Levinson, mikakati ya upole huzuka ili kukabiliana na tishio la uso. Tishio la uso ni vitendo ambavyo huingilia matakwa ya uso wa msikilizaji. Hivi ndivyo nadharia ya upole ilivyoanzishwa (asisiwa) na Lachoff na kuendelezwa na Brown na Levinson itakavyotumiwa kuchanganua miiko na tasfida katika lugha ya Warabai na Waswahili.

Ni kutokana na nadharia ya uso ambapo nadharia ya upole ilizuka ili iokoe uso kutokana na matendo ya kuutishia uso ambapo husababishwa na miingiliano ya kijamii. Brown na Levinson (1978), wanasema dhana ya uso ni muhimu sana katika maingiliano na mawasiliano ya binadamu. Walitambua kuwa baadhi ya vitisho vyta uso vinavyotisha uso wa binadamu katika maingiliano yake na wenzake. Vitisho vyta uso ni vyta aina mbili yaani; ukosefu wa upole hasi na ukosefu wa upole chanya.

Ili kuwe na maelewano kati ya kundi au watu fulani wanaowasililiana, lazima lugha inavyotumika iwe na maneno ya heshima yenye kuonyesha upole na ishara zenye kueleweka vyema.



### **Mkakati wa rekodi**

Kuna mkakati ambao unaitwa, *kuwa nje ya rekodi*.

Huu ni ule mkakati unaotumia mafumbo na njia ya mzunguko kuelezea jambo fulani ambalo ni mwiko kwa Warabai na Waswahili. Ni mwiko kufichua kwamba mtu ana

Ukimwi kwa Kirabai. Kwa hivyo badala ya kusema mtu ana Ukimwi utasema “walumwa ni mbuzi” aliumwa na mbuzi. Kumaanisha mtu anayetajwa ana Ukimwi na hana tumaini la maisha. Hii ni kwa sababu mti ukiliwa na mbuzi hupoteza maisha.

Mkakati mwingine wa rekodi ni ule wa, *kuwa kwenye rekodi*.

Huu ni mkakati unaotumia njia ya upole kurekebisha tabia ya mtu fulani.

### **Kanuni ya upole**

Kando na kanuni ya ushirikiano, kuingiliana kwingi kwa tawaliwa na upole. Hii ni kulingana na tabia za kijamii za upole katika utamaduni wa watu fulani. Kanuni ya upole, ni mfululolizo wa kanuni ambazo Leech amezipendekeza kama njia za kuelezea vile upole hutumika katika mawasiliano.

### **Kanuni za Leech**

Leech (1987) anafafanua upole kama hali ya tabia ambayo humruhusu mhusika wa mawasiliano kujihusisha na mwingiliano wa kijamii katika mazingira mazuri. Katika kuelezea kanuni zake Leech anatumia maneno yake kwa aina mbili za ilokusheni. Anaita uwakilishi wake kama wakulazimisha, na anaita maagizo kuwa vinyume.

Kila kanuni inafuatiwa na kijikanuni ambacho si muhimu sana. Kanuni zote zaunga mkono lile wazo kwamba upole hasi ni muhimu kuliko upole chanya. Sio kanuni zote zina umuhimu sawa. Kwa mfano, hekima hushawishi kuliko ukarimu, ilihali idhini ni bora kuliko sitaha. Wazungumzaji waweza kutumia zaidi ya kanuni moja ya upole wakati

mmoja. Mara nyingi kanuni moja huwa mbele ya matamshi ilihali kanuni ya pili ni ya kuhusishwa au yakushirikishwa.

### **Mikakati ya uso na upole**

Uso unamaanisha hisia za mzungumzaji katika kujitambulisha katika jamii. Mazungumzo yoyote yaweza kuingia katika hisia hii na huweza kutishia uso. Wazungumzaji wana mikakati ya kupunguza hili tishio la uso. Upole chanya wamaanisha kumsifu na kuwa mkarimu kwa msikilizaji. Upole hasi hupatikana katika njia nyingi za kupunguza hisia kutumika.

Nadharia hii inasisitiza kwambu lugha itumiwe vizuri bila kumkera mzungumzaji na msikilizaji. Pia ni matumizi ya lugha ki ungwana bila kukera hadhira. Kwa mfano, badala ya kusema “naenda kunya” utasema, “naenda msalani”.

Miiko hukataza matumizi ya lugha ya kueleza mambo ya siri, au nyeti waziwazi. Warabai huita Ukimwi, “Ukongo uriokudza”, yaani ugonjwa uliokuja”, lakini Waswahili huita Ukimwi bila kuuficha. Tamaduni nyingi hutumia lugha ya kistaarabu na Kirabai kikiwa mojawapo. Tamaduni nyingi husema viwango tofauti vya jamii ndio hutumia utaratibu huu kuzingatia umri, sherehe fulani, hafla ya upole, cheo cha mtu, madaraka ya mtu, madhumuni kama vile Shehe wa Kiislamu, mahusiano baina ya watu kwa mfano, mtu na mkaza mwanawе.

Nadharia hii ya upole inafaa utafiti huu wetu kwa sababu miiko ni mambo yahusuyo ustaarabu, kuepuka kukera wasikilizaji ambayo nadharia hii inasisitiza. Kuthibitisha umuhimu wa utafiti, miiko imefanyiwa utafiti juu ya Wameru na Mwito (2011), ambaye ni mbantu lakini ulikuwa wa kijuujuu, ambapo tuliamua kufanya utafiti miiko ya wabantu tukijikita kwa Warabai na Waswahili uwe wa kulinganisha na kindani.

### **1.8 Yaliyoandikwa Kuhusiana na Mada**

Ni muhimu kuangazia kazi za wataalamu wengine ambao kazi zao zafanana na utafiti wetu na zinazochangia kufahamika vyema kwa nadharia tulioitumia. Wasomi wengi wamezungumzia mambo yanayohusiana na mada hii yetu. Wengine wameongea kwa kijumla juu ya miiko na wengine juu ya miiko na tasfida katika jamii tofauti tofauti [wanavyoyatumia katika hali hii,] Harry (1954), anasema, “lugha huwakilisha utamaduni wa jamii.” Kwa hivyo, kuna uhusiano baina ya lugha na utamaduni wa lugha inayotumiwa.

Mwiko ni jambo la kiisimu jamii ya kijamii, hushughulika na uhusiano baina ya lugha na utamaduni ambamo miiko na tasfida zimo. Jambo hili huonyesha kuwa utafiti wa lugha huonekana katika utumizi wake na kazi yake katika hali ya kuleta uelewa wa utamaduni, imani, desturi na thamani ya jamii.

Nadharia tulioitumia msingi wake umejikita katika nadharia ya Pragmatiki. Nadharia hii yahusika na jinsi maana za maneno hujitokeza katika usemi, bali sio katika sentensi. Pragmatiki imefafanuliwa kama tawi la Isimu jamii inayoshughulika na uchunguzi wa

lugha katika mkitadha. Mkitadha upande mwingine ni hali ya mazingira ambayo matamshi hutolewa. Ni utafiti wa uhusiano baina ya lugha na mkitadha ambapo mazungumzo hutokea kisarufi. Katika msingi tunaangalia nadharia ya Grice (1973) ya umanisho na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987). Tunajumlisha na mikakati ya Maximu kama inavyotumiwa na Leech.

Nadharia ya upole itasaidia kufafanua vile tasfida inavyotumika kama mikakati ya upole, ilihali nadharia ya Grice itaongoza kutathiminiwa kama habari itolewayo ina matumizi ya tasfida na inawasilisha mawasiliano vyema. Kazi yake imechangia sana katika kazi yetu maana miiko na tasfida ya Warabai hutumia mikakati ya upole inapotumika katika mazungumzo ndio maana tukatumia nadharia hii.

Igboanas (2001), alisema, miiko ni umbo la utamaduni husika, hivi kwamba kilicho mwiko kwa utamaduni mmoja sio lazima kiwe mwiko kwa jamii nyingine. Dhana ya neno chafu, chukivu, ama lisilofaa huwa kwa utamaduni husika. Hii ndio maana tuliangalia miiko katika utafiti wetu wa miiko na tasfida ya Warabai na Waswahili.

Katamba (1985), anadhihirisha kuwa miiko imefunganishwa na utamaduni wa jamii. Hii imetusaidia kutafitia miiko na tasfida ya Warabai, na vilevile miiko na tasfida ya Waswahili- Wajomvu kwani miiko iko katika utamaduni ambao miiko yao imefungamana nao. Hymes (1954), anasema utamaduni ni jumla ya mitazamo, kaida, malengo ya kimaadili yanayotambulisha asasi na shirika au kundi fulani la watu. Hii inafungamana na utafiti wetu wa miiko na tasfida ya Warabai na vilevile ya Waswahil,

kwani miiko katika jamii ya Warabai, yalenga kudumisha maadili yanayotakitikana katika Warabai. Ndio sababu tulifafiti juu ya miiko natasfida ya Warabai na ya Waswahili. TUKI (1990), laeleza lugha kama mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii wenyewe utamaduuni unaofanana. Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa lugha huwasilisha utamaduni wa jamii husika kulingana na maelezo yaliyo tangulia ya TUKI. Utafiti huu ulihusu kuchunguza kuwepo kwa miiko katika Warabai na Waswahili.

Fromklin n. w. (2003), wanasema ya kwamba maneno mengine katika jamii huwa miiko, yaani, hayafai kutamkwa katika jumuia. Vitendo viliwyokatazwa huakisi mitazamo na mila za jamii husika. Maneno ya miiko mengine huweza kutumika kwenye mazingira mengine, yaani maneno ya miiko yanaweza kutegemea muktadha. Kwa mfano neno, “kojoa” katika Kirabai laweza kumaanisha kwenda haja ndogo, lakini ukimwambia mtu haswa mwanamke na wewe uwe mwanamme humaanisha ngono. Badala yake unaweza kutumia neno “kupigatsi”.

Ilihali Waswahili hasa Wajomvu wasemapo kukojoa humaanisha kwenda haja ndogo. Neno kukojoa halina maana nyingine kwa Waswahili. Bali lina maneno mengine mbadala yake kama vile neno “kushii” kwa kumwambia mtoto mdogo akojoe. Waswahili wakiongea juu ya mtu aliyeathirika na Ukimwi husema ana Ukimwi bila kutumia maneno mengine. Hawana neno la tasfida la Ukimwi. Wardhaugh (2002), anasema kutii miiko ni matumizi ya lugha ambayo ni kama kuivisha nguo lugha ionekane kuwa inapendeza na yenyе upole kwa msikilizaji. Katika Warabai ukitaka kumrejelea mtu mwenye Ukimwi,

mtu husema, “walumwa ni mbuzi” kwa Kiswahili maana yake ni “aliumwa na mbuzi ambayo husitiri uso wa anayerejelewa. Hii hupunguza ukali wa neno Ukimwi.

Kulingana na Mwito (2011), katika kazi yake ya tasnifu ya miiko ya Wameru, akimrejelea Trugdill (2002), asema kwamba katika lugha, mwiko hujihusisha na mambo ambayo hayasemwi hadharani, hayatendwi kabisa na hasa maneno ya kujieleza hayatumiwi kimazoea. Kwa hivyo iwapo maneno ya mwiko hayatumiki, basi hayawezi kubakia katika lugha kwa muda mrefu. Wakati mwingine maneno ya miiko hubakia katika lugha kwa kusudi la kuelezea hisia kali kame vile kitendo cha kujamiana kama vile kunajisi, badala ya kubaka. Maneno ya mwiko huweza kutumiwa na watu wa umri mmoja walio na ukuruba wa karibu sana kama bibi na bwana. Watu wa nasaba moja na umri mmoja huweza kutumia maneno ya miiko bila tisho la adhabu.

Ullman (2005), anasema kila utamaduni huwa na mambo ambayo hayafanywi wazi wazi (miiko), ambayo hujengwa na utamaduni husika. Hii inawiana na mada yetu, maana katika Warabai kuna mambo ambayo ni mwiko kutaja. Kwa mfano, badala ya kusema, “msichana amebalehe husema amevunja ungo (yumera ndugu). Waswahili husema msichana amebalehe bila kutumia njia ya mzunguko. Utamaduni wa jamii moja huweza kuwa tofauti na wa jamii nyingine, na kwa hivyo, mwiko kwa jamii moja waweza kuwa si mwiko kwa jamii nyingine. Waswahili (Wajomvu) wanaporejelea kijana mwenye umri kati ya miaka tisa hadi kumi na mbili, husema amebalehe. Hawana jina jingine la kuashiria msichana au mvulana aliye katika hali hii.

Katika kundi lugha la Warabai na vilevile Waswahili mwiko wa chakula, wanyama wasioliwa ni kama vile mnyama aliyekufa mwenyewe haliwi na baadhi yao ilihali Warabai wengine hula kwa sababu ya miegemeo ya kidini. Hii ni kwa sababu Warabai na Waswahili wengine ni waislamu, ambapo dini huwakataza kula nyama ya mnyama asiyechinjwa na muislamu bali amekufa mwenyewe. Lakini yule aaminiye dini ya kienyeji hakatazwi kula.

Fromklinna Rodman (1988:189), wanaangazia jamii katika mambo ya Isimu jamii ibuka kwamba hutunga maneno ambayo baadaye huweka mipaka baina ya yale yawezayo kusemwa kwa njia ya upole na yale yasiyoweza kusemwa, yaani, miiko. Wanasema kwamba maneno yote katika binadamu yaweza kutumika lakini jamii huweka mipaka ya ni wapi, lipi laweza kusemeka na lini. Wanazidi kusema kwamba uchafu, au uzuri wa lugha huwa kwenye masikio ya msikilizaji au katika jamii lugha fulani. Kuishi kwa mwanadamu kwa wema huleta vijidhibiti vyta matumizi ya lugha. Hii ni kweli kwani Warabai wana maneno ambayo hayawezi kutumika kila wakati lakini, wakati mwingine hutumika. Hususani ni maneno yatajayao sehemu nyeti za mwili. Haya huweza kutumika katika nyimbo za uombolezaji mtu anapokufa. Utafiti wetu walenga kuchunguza maneno ya tasfida kama sehemu ya vidhibiti vyta matumizi ya lugha.

Kulingana na Halliday (1978:123), lugha inatumika kama ishara ya kijamii kuleta maana kulingana na mkitadha kwa hivyo lugha ni mfumo wa maana ambao hubeba ukweli wa utamaduni. Kulingana na utafiti wetu wa miiko na tasfida ya Warabai Waswahili, dhana

hii inaafikiana sawa sawa. Warabai huita sehemu ya kiume ya siri mdudu (nyoka), kuiashiria kwamba sehemu hiyo ni kama nyoka huuma, ikimaanisha ngono.

Trudgill (2002:58), anasema katika jamii nyingi, maongezi ya wanaume na yale ya wanawake hutofatuiana. Pia anaendelea kusema kwamba lugha haitofatiani kinasaba, kikabila, kiumri, na kijinsia pekee bali katika muktadha ambamo mzungumzaji hujikuta. Pia tuliongozwa na nadharia ya Blutner [2000], ya Pragmatiki, ambayo hushughulika na kuchunguza michakato ambayo hufanya maana ya kiisimu ya neno iliyo wazi kubadili katika usemi kwa mfano, *walumwa ni mbuzi*. Mbuzi ni mnyama wa kufugwa ambaye si kawaida kuuma mtu. Huweza kumaanisha, Ukimwi litumiwapo. Waswahili wakirejelea mtu anayeugua ugonjwa wa Ukimwi husema mtu yule ana Ukimwi ilihali Warabai hutumia maneno ya tasfida kama vile “*waliumwa ni mbuzi*” kumaanisha aliumwa na mbuzi kwa Kiswahili.

Pragmatiki leksika huwa na jukumu la kuchunguza jinsi maana za maneno zilizopambanuliwa kiisimu hukubalika kutumiwa katika matumizi ya lugha au usemi katika miktadha mbalimbali. Msamiati wa miiko hurejelea maana ya maneno au usemi wa kimsingi. Maana huambatanishwa na muktadha bila kurejelea maana asili ya neno au usemi. Kwa hivyo tulichagua nadharia ya upole, kwani hii ndio itafaa kuchanganulia misamiati ya miiko na tasfida kwa kuwa misamiati au maneno haya hutumiwa kulingana na mkitadha. Baadhi ya kazi tulizopitia ziliweka wazi kuwa hakuna watafiti wengine Warabai waliotafiti kuhusu tasfida katika msamiati ya miiko, hii ilitusaidia kuelewa

utafiti wetu na kujaza pengo hilo. Qadi [2009], anasema kwamba dhana ya tasfida ilitokana na neno la Kigiriki limaanishalo sauti nzuri au ya kuvutia, au ya kupendeza.

Alimnukuu Wilson [1993], ambaye alichukulia maneno ya tasfida kama maneno mbadala ya yale ambayo ni ya matusi au machafu. Wazungumzaji wasemapo mtu mkubwa humaanisha mzee.Tasfida kulingana na Qadi hugawanyika kuwili, hasi na chanya. Maneno ya tasfida hutumika kwa jumla katika uadilifu katika jamii ambayo huashiria ushirikiano na hadhira. Kulingana na Qadi, tasfida huchukuliwa kama mambo muhimu katika kila lugha, na lugha isiyotumia tasfida huchukuliwa kuwa chombo punguani cha mawasiliano. Kwa hivyo hutumiwa kuepuka yale hayatakikani kutamkwa au kuandikwa. Utafiti wetu ni tofauti na ule wa Qadi kwani wetu si wa kulinganisha, hata hivyo Warabai nao hutumia tasfida hasi.

Nguti (2013), alifanya utafiti kwa kulinganisha matumizi ya tasfida juu ya Kikamba na Kiswahili katika matumizi katika mazingira ya nyumbani. Hamu ya kufanya utafiti ilitokana na Stockwell's (2008), kwamba kila jamii hung'ang'ana kuleta uadilifu katika jamii kwa kutumia maneno ya tasfida nyumbani.Kando na kwamba utafiti wake ulikuwa wa kulinganisha, ulionyesha kuwa tasfida ni chombo muhimu katika mawasiliano ya kijamii.

Hitimisho la utafiti lasema, ingawaje jumuia huwa tofauti lakini manufaa na mazingira hufanana. Data ya utafiti wa Nguti [2013], ilikusanywa kwa kutumia hojaji na mahojiano pale maoni ya wahusika yalitumiwa, na msingi wa nadharia ulikuwa ule wa upole kama

ulivyoendelezwa na Brown na Levinson [1978]. Utafiti wetu wa sasa unaafikiana na kazi ya Nguti kufuatana na msingi wa nadharia na mpango wa utafiti.

Utafiti wetu ingawaje uko tofauti na ule wa Nguti, wake ni wa ulingalinishi ilihali wetu si wakulinganisha bali niwa kuchunguza kuwepo kwa matumizi ya miiko na tasfida katika jamii ya Warabai walinganisha na ile ya Waswahili. Kando na hayo, lugha inayotafitiwa ni tofauti na ile tunayotafiti ingawajezote ni za kibantu. Kirabai kidesturi na kimila ni tofauti na Kikamba na Kiswahili. Tafiti hizi mbili zatofautiana kimipaka. Akiwa Nguti akizingatia mkutadha wa kijumuia, utafiti wetu uko juu ya magonjwa, vyakulavisivyoliwa, wanyama wasioliwa, Ngoni, Ndoa, Maradhi, Ukimwi, Kifo, Kubalehe, Kubaka na kama yanavyotumia tasfida katika Warabai na Waswahili.

Mbaya (2002), aliwasilisha utafiti wa ufanuzi juu ya mila za Waoromo (Ethiopia), ambazo huepuka kutaja majina ya watu wahusianao katika ndoa. Utafiti unaonyesha kwamba kwa sababu za kiisimu za miiko, bibi, bwana na wakwe huepuka kutumia majina yao, na huyabadilisha na aina zingine za maneno ya kubandika. Waafrika huwaita watu, hususani waliowazidi umri, kwa kutumia maneno ya tasfida. Utafiti ulichanganua maneno ya miiko na kuyaelezea kwa kutumia mikakati iliyotumiwa kubuni maneno mbadala. Hii pia yapatikana katika lugha ya Warabai na katika Waswahili.

Munyiri (2006), alitafiti juu ya lugha na jinsia juu ya lahaja ya Gi-Kabete ambayo ni mojawapo ya Kikikuyu. Lengo lake lilikuwa ni kuthibitisha kama msamiati wa Kikikuyu ina misamiati inayolingana katika sematiki na kwa kiwango gani misamiati yahusiana na

jinsia moja ilihali ikijaribu kutumisha jinsia kwa kugandamiza jinsia nyingine. Munyiri alijikita katika lugha na jinsia na vile lugha yaweza kuleta ubaguzi kwa wake kwa waume. Alithibitisha kwamba lugha ya ngono iko katika Wakikuyu kupitia wanawake na wanaume kufananishwa na chakula na wanyama. Kwa mfano njamba, kumaanisha jogoo, na nyanya kumaanisha mboga. Katika lugha ya Wakikuyu ya ngono wanawake huonekana kama wasioenyesha ukakamavu ilihali wanaume huonekana wenye kupenda ngono.

Katika kazi ya Munyiri, dhana ya tasfida ulichukuliwa kama kitu cha ziada. Kulinganishwa na utafiti wa Munyiri, huu wetu wa sasa wachukulia tasfida kama nguzo kuu ya utafiti. Utafiti wa Munyiri na wetu ultofautiana kimipaka na mbinu ya utafiti. Utafiti wetu watumia nadharia ya upole ilihali ule wa Munyiri watumia nadharia ya misemo ya kijamii kuchunguza data.

Wambua (2009), utafiti wake ulikuwa juu ya tasfida na maneno ya miiko ya Kikamba. Utafiti wake ultafiti maneno ya miiko ya Kikamba kwa kulinganisha tasfida za lahaja ya Machakosi na tasfida na miiko ya Kikamba cha Kitui. Pia alichunguza hisia tofauti zilizoibuka kati ya lahaja hizi mbili kupitia matumizi ya maneno ya tasfida na miiko. Utafiti wetu wa sasa wafaidi kutoka kazi ya Wambua kutokana na mbinu za utafiti.

Wambua alitumia mahojiano na hojaji kukusanya data, na sisi tutatumia mbinu sawa na hiyo kukusanya data. Ingawaje kazi ya Wambua yatofautiana na utafiti wetu katika mipaka, kwani utafiti wetu umechanangua maneno ya tasfida na miiko ya lahaja ya

Kirabai na shauku kuu ni tasfida na miiko juu ya magonjwa-Ukimwi, ngono, kubaleghe, kifo, vyakula visivyoliwa, wanyama wasioliwa, ndoa, kwenda haja.

### **1.9 Mbinu Ya Utafiti**

Utafiti huu unahu sehemu mbili, katika maktaba na nyanjani. Maktabani tulitumia kwa kwenda kutafuta na kusoma kazi zinazooana na utafiti wetu. Vile vile tulidurusu vitabu vya nadharia ya upole. Pia tulidurusu juu ya dhana ya tasfida ili tuweze kubainisha inavyodhihirishwa katika msamiati wa miiko na tasfida ya Warabai na vilevile juu ya Waswahili lahaja ya Wajomvu. Katika harakati zetu za utafiti tulienda nyanjani. Utafiti huu wa nyanjani ulifaa. Ulifanywa katika eneo la wilaya ya Rabai ambako tulichagua sampuli za wanaume na wanawake. Mahojiano na ushirika zilitumika nyanjani kuwahoji wahojiwa, sampuli za watafitiwa viwango tofauti tofauti vya elimu, umri, dini, wanaume na wanawake zilitumiwa.

Kwa kuwa maswala ya miiko na tasfida ni maswala nyeti katika jamii, mtafiti aliwatumia watafitiwa ambao walikuwa wa umri mkubwa zaidi yake, waliojua mambo ya miiko na tasfida ya Warabai na Waswahili vyema [na kuwahoji]. Walikuwa wazawa wa Rabai na waelewa lugha ya Kirabai na Kiswahili, mila na desturi za Warabai na zile za Waswahili. Tulihudhuria mazishi ili kushuhudia uvunjaji wa miiko kupitia nyimbo za uombolezaji za Warabai na kulinganisha na zile za Waswahili. Tulichagua sampuli ya watafitiwa ishirini ambao pia ni wazawa na watumizi wa lugha ya Kirabai kama lugha yao ya kwanza. Watafitiwa walikuwa wa umri kati ya miaka ishirini na sitini. Tulichanganua na kutathmini data kwa kuzingatia mikakati ya pragmatiki lekiska ya

Blunter (2000) na ile ya uhusiano, inayohusu jinsi maana za maneno hufasiriwa katika miktadha mbalimbali.

Tulitumia hojaji na mahojiano ya moja kwa moja. Pia tulitumia mahojiano ya ushirika ambapo tulienda pale vitendo vya uvunjaji miiko vilitokea nyanjani. Utafiti ulifanywa katika kata ndogo ya Rabai na JomvuKuu Gatuzi dogo la Mombasa. Nilitumia ushauri kutoka kwa wahadhiri walio wasimamizi wangu na hata wahadhiri wengine katika Idara ya Kiswahili katika ufanisi wangu wa shughuli nzima ya utafiti.

Watafitiwa ni wazungumzaji wa Kirabai na wazungumzaji wa Kijomvu na vilevile Kiswahili kama lugha zao za kwanza. Kwa hivyo walitumia uwezo wao wa kutumia lugha za Kirabai na Kiswahili kufanya utafiti huu wa miiko na tasfida ya Warabai na kulinganisha na ile ya Waswahili. Mtafiti vile vile alitayarisha hojaji na ratiba juu ya mada ya miiko na tasfida ya Warabai na kulinganisha na ile ya Waswahili. Pia alitumia mahojiano ya shirika kama njia ya ukusanyaji wa data. Mipango au ratiba za mahojiano na hojaji zilitayarishwa katika lugha zote mbili za Kirabai na Kiswahili. Alitumia sampuli, kwani mtafiti hangeweza kuhoji watumizi lugha wa Kirabai na Kiswahili wote katika utafiti, pia hakuwa na hakika kama watu aliochagua wangekubali kuhojiwa.

Hojaji ni njia mwafaka ya ukusanyaji wa data, ikizingatiwa hoja ya mada ya miiko inayotafitiwa. Mwelekeo huu unaungwa mkono na Marshall na Roseman [1999], ambao walisema hojaji hutumiwa kukusanya habari kuhusu mambo katika jamii. Utafiti ulikusudia utafutaji wa habari kuhusu maneno ya miiko ya lugha ya Warabai ambazo

watafitiwa wanaziona kuwa za kuaibisha katika mahojiano ya ana kwa ana.Vilevile utafiti wahusiana na maneno ya miiko na tasfida ya lahaja ya Kijomvu ambayo ni mojayapo ya Waswahili. Ubora wa utumizi wa hojaji ni kwamba sampuli kubwa yaweza kufikiwa Mahojiano ya moja kwa moja,umuhimu wake ni kwamba mtafiti aweza kuwasiliana na wahojiwa ili kupata habari za kuaminika kwa data iliyohitajika kutoka kwa wahitajika. Kama habari haikupatikana kwa mhojiwa ya tasfida ya neno fulani au misemo, mtafiti angemhoji mtu mwingine na kuipata.

Mtafiti alitumia uchunguzi kama njia ya utafiti, faida yake ikiwa uchunguzi humsaidia mtafiti nafasi ya kupata data kutoka matukio halisi ya kijamii. Mtafiti anaweza kuchunguza yale yanatokea kuliko kutegemea habari ya kusimuliwa na mtu mwingine. Mtafiti kuititia uchunguzi aliweza kupata tabia za mtafitiwa.Mbinu hii ilimwezesha kutazama na kushuhudia wazi utumizi wa maneno ya tasfida katika halisi kama vile kwenye mazishi na maombolezi.

### **1.10. Hitimisho**

Katika sura hii ya kwanza tulianza kwa kuelezea juu ya mada ya utafiti wa Warabai juu ya sehemu wanapopatikana, asili yao na shughuli zao za kila siku na vilevile Waswahili (Wajomvu) shughuli zao za kila siku na wanakopatikana na kulinganisha.Tumelezea tatizo la utafiti na madhumuni kwa kujikita katika nadharia tete tulizoziteua.Pia tumeelezea sababu za kuchagua mada, halafu tukazieleza kuhusu upeo na mipaka ya utafiti. Tumezungumzia juu ya msingi wa kinadharia ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti.

## **SURA YA PILI**

### **MIIKO NA TASFIDA**

#### **2.1 Utangulizi**

Maneno ya miiko na tasfida katika lugha yoyote ikiwa pia Kirabai na Kiswahili humsaidia mnenaji kusema vitu ambavyo havisemeki kwa kutumia mikakati ya upole. Katika sura ya kwanza tulieleza yalioandikwa kuhusu miiko na tasfida. Katika sura ya pilii tulifasili maana ya miiko, tulionyesha vile miiko ya Warabaina Waswahili iko katika jamii ya Warabai. Tulielezea aina ya miiko ya jamii lugha ya Warabai na vile vile Waswahilina maneno ya tasfida yanayotumika kama mbadala ya yale ya miiko.

Maneno haya ni muhimu kwani yatakuwa msingi wa utafiti katika sura ya tatu na nne. Maneno ya miiko ya Warabai na Waswahili yamelindwa kwa kutumia upole kwenye jamii ingawaje ni mambo yenyeye kuelekeza jamii. Ullman (2005), anasema kila utamaduni huwa na mambo ambayo hayafanywi wazi (miiko), ambayo hujengwa na utamaduni. Lakini hutumia tasfida kuyataja. Kwa mfano, badala ya kusema msichana amebaleghe, tunasema amevunja ungo.

#### **2.2 Fasili ya Mwiko**

Kuna maelezo tofauti tofauti kuhusu asili ya neno mwiko, huku maelezo mengine yakiwa na misingi ya anthropolojia, ambayo hueleza mwiko kama swala la ung'amuzibwete ambalo limekuwepo tangu zama na hurithishwa kizazi hadi kingine.

Mwiko ni jambo ambalo limekatazwa katika jamii, linalohusiana na vitendo vyatyanajamii au mila za jamii husika, ambazo huhusu dini au tamaduni na imani za dini. Neno mwiko ni tafsiri ya neno, Kitonga “tabu” ambalo humaanisha lililokatazwa, ambalo hutokea katika tamaduni nyingi za Palensia kusini mwa Bahari Pasifikasi.

Matumizi ya dhana mwiko katika lugha ya Kiingereza yalianza mnamo 1777 wakati mtafiti Captain James Cook alizuru Tonga ambako alipata kusikia neno “taboo” mara ya kwanza, kwa jumla miiko ya tamaduni nyingi ni ile iliyohusu maradhi,kifo,vyakula, ngono na kubaleghe. Lengo la sura hii ni kuwafahamisha wazungumzaji wa lugha ya Kirabai na wasio Warabai na wasiozungumza lugha ya Kirabai au Kiswahili dhidi ya kutumia lugha ya kuudhi kuhusiana na miiko. Watajifunza maana za maneno na misemo iliyokatazwa katika jamii na yale ambayo yamependekezwa yasitumike katika lugha hiyo.

Sura hii kwa hivyo, inatoa maneno ya tasfida ya yale ya miiko kuyatajia katika lugha ya Warabai na vilevile Waswahili kwa upole.

### **2.2.1 Uhusiano baina ya Miiko na Tasfida**

Kuna maelezo mengi tofauti yahusuyo chanzo cha maneno ya miiko, ambapo maneno mengine ni ya ufanuzi wa kielemu ya maendeleo ya mwanadamu. Mengine ni ya kufikirika au mawazo ambayo yaeleza miiko kama mambo ya mwanadamu, kuna mengine ni ya kiakili au mawazo ambayo yaelezea miiko kama mambo yapokezwayo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kando na kuwepo kwa maelezo tofauti tofauti kwa

ajili ya maneno ya miiko, inakubalika kwamba kuwepo kwa miiko ndio huibua matumizi ya tasfida, ambayo ni maneno yenyе staha.

Fromklin, Rodman na Hymes (2003:476), wanasema kuwa, “maneno mengine katika jamii zote huchukuliwa kuwa miiko, hayatakikani kutumika.” Wanasema kwamba neno “mwiko” lilitumiwa Tongan, ambapo katika lugha ya Kipolynesia lamaanisha vinavyo katazwa. Hii ya maanisha watu hukatazwa kufanya vitendo kitu ambacho ni mwiko na pia hukatazwa kukizungumzia. Maneno ya miiko mengine huweza kutumika katika miktadha mengine na yakatazwa kutumika katika miktadha mengine. Hii ni kweli katika wazungumzaji wa Kirabai na vile vile Kiswahili.

Maneno ya matusi yahusuyo sehemu nyeti za binadamu ni mwiko kutajwa hadharani. Lakini wakati mwingine hutumika katika miktadha mengine kama vile kwenye uombolezaji, mtu aagapo dunia na hata matangani katika jamii ya Warabai na Waswahili. Kwa mfano, kuna nyimbo zinazosheheni matusi ambazo kwa kawaida haziimbwi ovyo ovyo lakini hutumika kwa maombolezi katika jamii ya Warabai mtu afapo.

Mfano wa wimbo, *chimbwambwa mbolo ni dzogofya, chimbwambwa mbolo ni dzogofya*. Chimbwambwa ni jina la mtu anayeelezwa kuwa mbolo—sehemu ya ume ya uzazi kwamba ni kitu cha kutishia watu, hususani wanawake. Ambapo nyimbo hii haiwezi kuimbwa pahali popote isipokuwa kwenye maombolezi na matanga pekee. Watu hupendelea kutumia maneno ya tasfida kutaja sehemu nyeti za uzazi. Kwa mfano utasikia mama akimwambia mtoto wa kiume atoe mnyama akojoe asije akakojolea suruali.

Wardhaugh (2002:238), anasema matumizi ya maneno ya tasfida hulenga kusitiri mambo fulani katika lugha juu ya hali fulani ya maisha ili kufanya yaweze kutumika vizuri kwa upole na kutumika hadharani. Na hivi ndivyo Warabai hufanya. Kwa hivyo kazi ya Wardhaugh imetufaa sana.

Maneno ya tasfida na misemo huturuhusu kuongea juu ya mambo ambayo hayafurahishi na husaidia kuziba aibu. Mfano ni mambo yahusuyo ugonjwa, kifo na ngono. Pia mambo ya tasfida yaturuhusu kutumia, kutambulisha au kuelezea mambo chukivu katika lengo la kufanya mambo yaweze kuvutia. Kwa Warabai kifo ni mwiko kutajwa waziwazi. Hutajwa na watu wachache hadharani na hutumia maneno mengine ya tasfida kuashiria kifo. Kwa mfano, Warabai husema, “yuhuricha, yubanangika, yuphirika chiko, yaani yuhuricha-ametuacha, yubanangika ameharibika, yuphirika chiko—amepeleka kiko ambacho ni chombo cha kuhifadhia tumbaku (ugoro). Hii hupunguza hisia za muathiriwa na kifo ilihali Waswahili husema (ametuacha) kumaanisha kifo. Waswahili mtu afapo husema amefariki, mungu amemukhtari ama, ameacha dunia, pia husema amekufa. Hii huonyesha kwamba wana maneno machache ya tasfida kuhusiana na kifo kuliko Warabai.

Trudgill (200:18), aeleza kwamba katika lugha, mwiko wahusiana na mambo ambayo hayazungumziwi, na hasa mambo ya kawaida, ambayo kama hayatumwi kabisa basi hayataweza kubakia katika lugha. Aliendelea kusema kwamba watu watumiao maneno ya miiko huwa hawajui kuwa ni miiko na ni kwa nini ni miiko isipokuwa kwamba ni miiko na kubakia katika lugha kuleta hisia kali.

Fromklin, Rodmanna Hymes (2003:478), wanaeleza kuwa miiko ni maneno mawili, au zaidi, au misemo inayoweza kuwa na maana sawa kilugha, ambapo moja hukubalika na lingine kutokubalika. Utafiti huu unakubaliana na waandishi tulowanukuu kwamba kilugha hakuna sababu maalumu kwamba neno moja liwe zuri na lingine liwe baya. Jambo ni kwamba mila ndio hutoa uamuzi kuwa lipi ni sawa na lipi si sawa. Watu husema kuwa ameenda mbele za haki badala ya kusema amekufa. Hivi ndivyo mila huruhusu matumizi ya tasfida. Si jambo jipya. Inasemekana mwana historia wa Kiyunani Plutarch [karine ya kwanza] alisema kwamba Wayunani wa kale walisema kwamba waliweza kuziba mambo ya aibu kwa kutumia maneno ya staha kwa kuyapa maneno ya upole. Waliwaita Malaya; waenzi, kodi – mchango, na jela – chumba cha kulala.

### **2.2.2 Uhusiano baina ya Mila za Kirabai na Kiswahili na Miiko Kilugha**

Lugha hazitofutiani kiurithi bali kimatumizi katika uwezo wao wa kubadilisha taratibu za matumizi ya lugha. Taratibu za matumizi na uwezo wao hubadilisha taratibu za matumizi ya lugha ambazo huongozwa na mila, utamaduni na desituri na historia ya jamii lugha. Miiko kilugha ni marufuku ya matumizi ya maneno yaonekanayo kuwa hayapendezi kutumiwa na kundi, mila au jamii fulani. Ingawaje, mila za Kirabai huruhusu matumizi ya maneno ya miiko katika miktadha kama vile mazungumzo baina ya watu wa tabaka moja au rika moja au watu ambao wamezoweana ama katika sherehe za matanga watu wa rika moja huvunja mwiko bila madhara yoyote.

Wajomvu ambao ni Waswahili hawatumii maneno ya miiko ovyo ovyo. Ni wastaarabu sana huepuka mambo yaletayo hisia kali yatajwapo. Hawatumii maneno ya miiko katika

hali ya uombolezaji kama vile Warabai hufanya. Nyimbo za uombolezaji huimbwa na wanawake na wanaume katika jamii ya Warabai. Ilihali ni wanawake tu wa Kiswahili ambao huimba nyimbo za dua Mswahili afapo.

Utafiti huu uligundua kwamba katika nyimbo za maombolezi zilizoimbwa na waombolezaji, maneno ya miiko yalitumika bila wasiwasi wala madhara yoyote. Pia nyimbo za harusi za kitamaduni zilitumia maneno ya miiko bila kujua, mfano wa wimbo wa harusi – *yanga yanga- yanga yanga ooh owayangayanga ohowa wahala Mkamba Mwamadi wa Tsuma, mchetu watumbo unaye be ndakala mjinga nawe.*

Tafsiri ni kwamba Mwamadii wa Tsuma alioa mwanamke kabilia la Kikamba ambaye alikuwa ametiwa mimba na mtu mwingine. Jambo ambalo lamfanya aonekane mjinga. Hapa ametumia maneno ya kumkejeli mwenye kuoa mwanamke ambaye si bikira. Vile vile yaonyesha kwamba ni makosa kwa Mrabai kuoa mwanamke asiyekuwa wa kabilia lake.

Katika sherehe hizi nyimbo au mashairi yenyewe maneno ya matusi hutumiwa bila kuwa na madhara yoyote kwa mzungumzaji na vile vile msikilizaji. Wakati mwingine usiokuwa wa sherehe kama hizi huwa ni vibaya kuimba nyimbo kama hizi. Kupitia kuja kwa ukristo na usasa, sherehe za kitamaduni zimetupiliwa mbali lakini hata hivyo katika jamii ya Warabai miiko bado ipo, ingawaje usasa umepunguza matumizi ya nyimbo za harusi na maombolezi za Kirabai ya mara kwa mara. Hii imeleta utata wa je! Miiko itabaki kuwepo au itapotea katika lugha. Wajomvu walipiga goma liitwalo tutu wakati wa harusi

na maulidi. Ambazo ni nyimbo za dini ya Kiislamu ambazo hazisheheni matusi kama zile za Warabai na kukejeli watu. Warabai hutumia msemo “walumwa ni mbuzi” kumaanisha mtu ana Ukimwi ilihali Wajomvu husema moja kwa moja ana Ukimwi.

### **2.3 Asili ya Miiko na Tasfida Katika Jamii ya Warabaina Waswahili**

Tasfida zitumiwazo na Warabai zatokana na mambo ya kila siku ya jamii lugha na wakati mwingine kutoka asili zingine. Utafiti huu uligundua kwamba wazungumzaji wa Kirabai hutoa maneno ya tasfida kutoka matumizi ya lugha ya kawaida kwa mfano, ugonjwa wa Ukimwi umpatapo mtu husemekana, “walumwa ni mbuzi,”tafsiri - aliumwa na mbuzi, ili kuepuka kutumia maneno yenye hisia kali kwa mwathiriwa wa Ukimwi. Hii hupunguza ukali na hofu iambatanayo na ugonjwa wa Ukimwi.

Ilihali Waswahili husema kuingiliana na mtu au mke wake mtu kumaanisha ngono. Pia hutumia neno kujamiana, na hata msemo kutangamana kwa starehe ya kitandani, kumaanisha ngono. Mtu apendaye wanawake sana huitwa kapera hasa akiwa hajaoa. Na mwanamke apendaye wanaume huitwa shangingi. Mswahili akikatazwa tendo la ngono husema nimekatazwa ngono.

#### **2.3.1 Kijamii na Hali ya Matumizi ya Kawaida ya Lugha**

Chochote katika mazingira chaweza kutumiwa kama tasfida ya kile ambacho ni mwiko. Warabai wana uwezo wa kubadilisha maneno ya kawaida na dhana tofauti tofauti kuwa tasfida. Dhana hizi hutokana na mazingira, haswa yale yahusuyo matendo ya ngono. Kwa mfano, neno la Kirabai litumiwalo kutaja matendo ya ngono ni *kumwinjira, kutsembera*

*na mkaza mtu*—kumwingia, kutembea na mke wa mtu. Hutumika ili kupunguza ukali, hisia au kutaja mambo ambayo ni mwiko yahusuyo ngono. Sehemu ya uume huitwa mnyama, jongoo, mdudu. Mwanamume mwenye sifa za kupenda wanawake huitwa kajogolo yaani jogoo. Maana jogoo hupenda kufanya ngono na kuku wote, habagui yeze hufanya ngono na hata mamake.

Sehemu ya mwanamke ya uke huitwa mvumvu yaani uchi wa mwanamke. Hii kwa mtu mwagine ambaye yuko nje ya hayo mazungumzo huchukulia ni mambo ya kawaida. Lakini anapozingatia yasemwayo kwa makini hugundua kuwa mazungumzo yanayozungumziwa ni mambo nyeti. Katika sitiara kuna kufanana baina ya kile kimemaanishwa na hadhira na mzungumzaji wa mambo katika jamii husika.

Mdudu katika hali hii ya mazingira hutumika kama tasfida ya sehemu nyeti ya mwanamume. Hii sehemu ya mwanamume imefananishwa na mdudu ambaye kawaida huuma watu. Kwani kufanya ngono kumefananishwa na kuuma kwa mdudu. Pia humaanisha kwamba mwanamume katika ngono huwa anashughulika sana kuliko mwanamke ambaye huwa hachukui hatua ya kuomba mwanamume kufanya ngono naye. mwanamke huwa haonyeshi nia ya kufanya ngono bali mwanamume huweza hata kutamka kwamba ataka kufanya ngono bila wasiwasi wowote ajisikiapo kufanya hivyo.

Maneno ya tasfida yatokanayo na mazingira ya mzungumzaji ni maneno kama (*vvvvv*) yaani tupu kumaanisha uchi wa mwanamke hauna sura maalum ilihali mdudu husimamia uchi wa mwanamume ambao hufanana na mdudu (*nyoka*). Mtu atakayekuzungumzia juu

ya kufanya ngono ungesikia akisema *wanikahazayuuu*-yaani alikataa kushiriki ngono naye. Maneno uchi na mnyama yatumika kisitiara kumaanisha uume na uke. Hii hupunguza hisia za viashiriwa katika hadhira ya halaiki ya watu.

### **2.3.2 Kanuni za Matumizi ya Miiko.**

Kuna kanuni zitumikazo na matumizi ya miiko.

Kanuni za matumizi ya maneno ya miiko ni pamoja na umri wa mzungumzaji, uhusiano baina ya watumizi wa maneno ya miiko, mazingira ya matumizi ya miiko na mwisho ni jinsia ya wahusianao na mawasiliano. Utaona kwamba mzungumzaji huweza kuvunja mwiko anapozungumza na mtu mwenye uhusiano wa karibu na wa jinsia moja na hata mtu aliye wa rika lake.

Hapa mtu anaweza kutumia maneno ya miiko hata bila wasiwasi au madhara. Aweza kuzungumzia mambo nyeti kama vile ngono, ugonjwa wa Ukimwi bila kutumia maneno mbadala kama vile maneno ya tasfida kutajia mambo nyeti. Mtu akiwa katikati ya watu wa rika lake waweza kumsikia akisema waziwazi, *ninenda nikakodzole*-naenda kojoa ambayo ni mwiko kutamkwa wazi wazi. Pale anazungumza na mtu anayemheshimu kama vile mkazamwanawe au mtu wa umri mdogo itambidi atumie lugha ya tasfida. Kwa mfano kama ataka kwenda haja ndogo, Kirabai atasema, "nikatsuphe mahe", naenda kutema mate kwa Kiswahili. Ilihali Waswahili huepuka matumizi au uvunjaji miiko. Ingawajje wakati mwingine huvunja miiko kama pale wasemapo waziwazi naenda kojoa badala ya kusema naenda haja ndogo katika muktadha usioegemea umri wa mzungumzaji na msikilizaji.

Maneno ya miiko yanaweza kutumika katika mazingira mahususi. Katika mazingira ya uombolezaji, utakuta mambo ya miiko hutumika waziwazi bila madhara kwa uso. Hii hutokea kupitia nyimbo za kuomboleza, hasa za jamii tunayoitafiti ya Warabai. Nyimbo za maombolezi husheheni maneno ya matusi ambayo kwa mazingira ya kawaida huepukwa kutajwa ovyo ovyo. Mfano ni nyimbo za maombolezi za Kirabai ‘*nagwira kanga nikamuye mayo aehee mbolo ina tsingo*’-imaanishayo kwa Kiswahili ni kwamba – nashika kanga nikampe mama mboronina shingo.

Hii inalinganishwa na ugumu wa kushika kanga na kifo. Yaani kifo ni jambo ambalo si rahisi kulielewa kama vile kumshika ndege aitwaye kanga ambaye hulala juu ya miti na pia hupeperuka. Hii inaleta hisia ya kifo kwamba si rahisi kukielewa. Lakini katika mazingira ya furaha au sherehe za furaha utakuta maneno ya tasfida yanatumika sana. Katika kanuni ya jinsia utakuta mtu hushindwa kuongea mambo nyeti akiwa anazungumza na mtu wa jinsia fulani tofauti na yake mfano mwanamume akiongea na msichana aliye baleghe. Pia kuna mambo ambayo watu wa jinsia tofauti hawawezi kuyasema kwa kuwa ni mwiko kufanya hivyo. Wanawake hawaruhusiwi kuanika nguo za ndani hadharani, maana ni mwiko kufanya hivyo. Waendapo kuoga mtoni huwa hawavui nguo zote, lakini wanaume na wavulana waogapo mtoni huvua nguo zote. Pia kuna maneno ambayo hayazungumzwi kwenye watu wengi. Warabai husema “hangani *kavalagwa*”–ambayo kwa Kiswahili ni kwamba mtu anpotakapokuondoka kwenye msiba huwa haagi. Maneno ya kuomboleza hayasemwi mahali ambapo hapakufa mtu, kama vile kwenye mazingira ya harusi.

### **2.3.3Kuombwa kutoka lugha za kigeni**

Utafiti huu ulithibitisha kwamba Warabai wakati mwingine walitumia maneno yaliyoombwa kutoka lugha za wageni waliotangamana nao, haswa Waswahili na Waingereza. Maneno yaliyoombwa hutumiwa kama tasfida au mbadala ya yale ya miiko baada ya kutohoholewa. Mfano ni msemo wa Kirabai -*mdzomba mche katsinza kuku*.

Tafsiri:-mwanamke aliye mwisilamu dini haimruhusu kuchinja kuku. Yaani kuna mambo ambayo mwanamke wa Kirabai na haruhusiwi kufanya, kama jambo ambalo hufanywa na mume pekee kama vile, kutopoa au kuanza kuchoma na kula mahindi ya shambani kabla bwana kufanya hivyo. Hii ni kwa utangamano wao na Waswahili Waislamu ambao hawali nyama ya mnyama asiyechinjwa na mwanamume wa Kiislamu.

Kithibitisho kingine cha maneno ambayo Warabai huyatumia kamatasfida ya yale ya miiko ni matumizi ya neno, “shuweni” lililoombwa kutoka Kiingereza “swine”. Hutumika mbadala ya neno mpumbavu ambalo ni mwiko kutumiwa na Warabai. Waswahili nao hutumia neno lililoombwa katoka Kiarabu “baradhuli” wakimaanisha mjinga au mpumbavu.

Kwa hivyo, kuepuka kuleta tishio la uso wa mzungumzaji na msikilisaji neno “shuweni” hutumiwa kumaanisha mtu ni mjinga kama nguruwe. Hii ni kwa maana maneno ya miiko yatumiwapo huonekana yenyе kutishia nyuso za wa wazungumzaji na wasikilizaji (Stockwell 2003), tishio ndilo humfanya mzungumzajikulibadilisha neno na lile lililoombwa kutoka lugha nyingine kwa sababu lililoombwa huonekana kuwa la upole.

Maneno yanayotumiwa kutajia ngono kama vile kufanya mapenzi yaliombwa kutokana na Waingereza [making love] kama ya tasfida badala ya yale ya miiko. Kwa mfano, Warabai husema “kulala na mkaza mtu”. Tafsiri yake katika Kiswahili ni – kulala na mke wa mtu. Waswahili hutumia neno kujamiana kumaanisha ngono.

Haya ni maneno ya tasfida yatumiwayo badala ya yale ya miiko ya Warabai yatokanayo na yale ya Kiingereza. Sleep with somebody’s wife’-kulala na mke wa mtu. Kulala ni jambo la kawaida kwa watu wote na kwa hivyo Warabai wanaposema kulala na mke wa mtu huonekana kuwa na upole.

### **2.3.4 Umuhimu wa miiko na tasfida**

Miiko natasfidaina jukumu muhimu katika jamii. Hutumiwa ili kudumisha mila na desturi za jamii husika, hudumisha utamaduni na heshima kwa jamii katika watu wadogo kwa wakubwa. Hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

### **2.4 Muhtasari na hitimisho la sura ya pili**

Katika sura hii tumeshughulikia uhusiano uliopo baina ya miiko na tasfida, pia sura hii imetoa uthibitisho mkubwa wa msamiati na misemo itumiwayo kama miiko kwamba hutokana na isimujamii au mazingira. Imeendelea kueleza kwamba lugha na utamaduni, pamoja na jamii ni vitu vinavyobadilika ambavyo hubadilika kulingana na desturi ziathirizo lugha. Haiwezi kutukia nje ya desturi bali hutokana na urithi wa kijamii na itikadi ambazo ndizo vigezo vyta hali ya maisha ya watu.

Kwa kuhitimisha, ufasiri na ubainishaji wa miiko utafaa kwa sura ya tatu. Utaturahisishia uwasilishaji na uchambuzi wa miiko na tasfida katika sura ya tatu. Ni muhimu kwa kuwa uwasilishaji na uchmbuzi wa data kwa kuzibadili kwa kutumia maelezo ya dhana na mfumo wa miiko katika jamii ya Warabai yametupambanulia jinsi miiko inajidhihirisha katika jamii, hasa vile nyenzo za kuendeleza misamiati ya miiko hujidhihirisha katika miktadha tofauti tofauti.

## **SURA YA TATU**

### **UWASILISHAJI MIIKO NA TASFIDA YA WARABABAI NA WASWAHILI**

#### **3.1 Utangulizi**

##### **Uwasilishaji na uchanganuzi wa data ya miiko na tasfida ya Warabai**

Katika sura hii tutashughulikia majukumu yanayoteklezwa na miiko na tasfida ya Warabai. Katika sura hii tutachanganua data ya msamiati na semi za miiko kwa kuzingatia kategoria za miiko zilizobainishwa. Data iliyokusanywa tutaiegemeza katika makundi yanayotumika.

Ufafanuzi utajikita katika mtazamo wa nadharia ya upole kama inavyofafanuliwa na Leech, Brown na Levinson (1978). Data tuliyokusanya tuliiwasilisha kwa kutumia majedwali na kuonyesha kila mwiko na tasfida yakekimatumizi ya Warabai na Waswahili kimuktadha, pia tuliweza kuonyesha mikakati tuliyotumia katika matumizi ya miiko kwa misingi ya nadhara ya upole.

#### **3.2 Uwasilishaji wa Data juu ya Miiko na Tasfida**

Maneno ya miiko na yale ya tasfida ya Kirabai na Kiswahili. Katika Warabai na Waswahili kuna marufuku yaliyopo juu ya misamiati ya miiko juu ya kifo, maradhi ya Ukimwi, kubaleghe, ngono, kubaka, vyakula visivyoliwa, wanyama wasioliwa na ndoa. Kwa hivyo watu wazungumziapo maswala haya hutumia maneno ya tasfida ili wasije fanya wasikilizaji kutahayari au kudhurika na matamushi haya. Utafiti huu unalenga

kupeana mwongozo juu ya maneno ambayo yaweza kutumiwa badala ya yale ya kuudhi au ya kutahayarisha umma katika lugha za Kirabai na Kiswahili kwa vizazi vijavyo.

### **3.2.1 Msamati wa Ngonon**

Kuna maneno ambayo hutumiwa na Warabai ambayo humaanisha ngono. Warabai hutumia tasfida kwa kutaja mambo ya ngono. Hutumia maneno ya miiko ya ngono kwenye mazingira ya maombolezi, kupitia nyimbo za Kirabai za maombolezi. Kwa mfano, utasikia wakitaja katika wimbo wa matanga –“mbolo ina tsingo” humaanisha mboo ina shingo. Utumizi wa maneno ya miiko kwenye sherehe ya uombolezaji hutumiwa na wake kwa waume. Kwani nyimbo hizi huimbwa na waume na wake katika hali ya maombolez. Katika Warabai, kuna maneno mengi yatumiwayo kumaanisha kitendo cha kujamiana, tuzingatie mifano ifuatayo ya data juu ya ngono.

#### **Jedwali-3.2.1 Warabai Juu ya Ngonon**

<b>Maneno ya miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kuhomba	Nongo
Kudunga	Nongo
Kukodzorera	Nongo

<b>Maneno ya miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kumhenda mche	Kumfanya mke
Kuonana chimwiri	Kuonana kimwili
Kumva mvumvu	Kumpatia uchi wake
Kumfula na chulo	Kumfua na kifulio cha nazi (mtalimbo wa chuma)
Kulala naye	Kulala naye
Kulala na mkaza mtu	Kulala na mke wa mtu
Kutsembera na mtu	Kutembea na mtu

Kulala uriri mumwenga	Kulala kitanda kimoja
Kufanya	Kumfanya
Kumguta	Kumgusa

Warabai hutumia maneno ya tasfida haya hapo kwenye jedwali kuzungumzia miiko ya ngono. Matumizi haya humpunguzia fadhaa na hupunguza vitisho vya uso wa msikilizaji. Njeri (2007), alichukulia ngono kama mchezo au tendo la kawaida. Kwa mfano kuna maneno yaliyotumiwa kama tasfida yafuatayo.

Warabai hutumia maneno ya tasfida hayo hapo kwenye jedwali kuzungumzia miiko ya ngono. Matumizi haya huwapunguzia wazungumzaji na wasikilizaji fadhaa na kuwapunguzia vitisho vya uso.

### **Msikilizaji.**

Njeri (2007) alichukulia, ngono kama mchezo au tendo la kawaida.

Kwa mfano, kuna maneno yaliyotumiwa kamatasfida yafuatayo:

Maneno ya miiko	Maelezo
Mtsadzigo wa baba na mayo	Mchezo wa baba na mama
Kurima / kufyeka	Kulima
Kwendesha farasi	Kuendesha farasi
Kupiga “press ups”	Kupiga “press-ups”
Kuteketyana	Kutekerenyana
Kukunana	Kukunana

Mtafiti aligundua kwamba Warabai walitumia maneno haya, kwani walichukuwa tendo la ngono kama kitendo kizito ambacho husababisha mimba au kuambukizwa magonjwa mabaya kama vile Ukimwi, na iwapo kupitia kufurahia kitendo hicho na msichana apate

mimba, wangesema “warya maharagwe achivumbirwa” yaani alivumbiwa kwa sababu ya mchezo.

Pia husema “wadzazwa” – alijazwa kumaanisha ana mimba. Yaani sehemu ya uume ilikatika ndani ya msichana mwashiriwa ndio – “wadzazwa”. Katika Biblia pia kuna maneno ya tasfida yatumiwayo ya ngono. Kwa mfano, Biblia hutumia maneno ya tasfida kuhusu ngono.

“Adam wamumanya mchewe” – Adamu alimjua mkewe, ya maanisha Adam alifanya tendo la ngono na mkewe. *Mwanzo 4:1 Adam achimumanya, naye achihenda tumbo, achimvyala Kaini, achiamba, nidzipata mhoho wa chilume, kwa Masihi.*

Adamu akamjua Hawa mkewe, naye akapata mimba, akamzaa Kaini, akasema, nimepata mtoto mwanaume kwa Bwana.

Mtafiti aligundua kwamba mhubiri alipokuwa akihubiri juu ya mambo ya ngono, alitumia maneno ya tasfida ili kuokoa uso wa msikilizaji. Kwa hivyo maneno yote ya tasfida hutumiwa katika msamiati wa ngono kuokoa uso wa mzungumzaji na msikilizaji.

### **Jedwali 3.2.2 Waswahili (Wajomvu)**

<b>Maneno ya miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Nongo	Tendo la uzinifu
Nongo	Kuingiliana na mke wako
Nongo	Kujamiana
	Kutangamana kwa starehe ya Kitandani

**Kulingana na jedwali ni dhahiri kwamba Waswahili hutumia tasfida kuhusiana na mambo ya ngono kama vile Warabai.**

### **3.2.2 Msamiaati wa mimba na kuzaa**

Baada ya tendo la ngono na mwanamke kupata mimba, kuna maneno ya upole yatumiwayo kutaja mambo haya. Mtafiti aligundua kwamba watu walitumia maneno mengi kuashiria hali hii. Kwa mfano walitumia misemo kama, “kudungwa”: wadzazwa:, alijazwa, “wavumbirwa”–alivumbiwa. Maneno haya hayawezi kutumiwa katika mazungumzo ya upole, kwani huchukuliwa ni yakutishia uso.

Yanatumiwa na vijana kwa vijana. Maneno mengine ambayo hutumiwa na Warabai kuashiria uja uzito ni haya yafuatayo:

#### **Jedwali 3.2.2 Warabai na Waswahili.**

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Tumbo	Mimba
Mimba	Nijanizito, anahimili mimba

<b>Maneno ya miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Mwamimba	Mjamzito
Lutsunga	Fura tumbo
Dzazi	Mjamzito

Mimba inapotimia, mtoto huzaliwa. Hiki ni kitendo kinachoheshimiwa, na mtu anapotaka kuongea juu yake basi hutakikana atumie maneno ambayo hayatishii uso. Kwa mfano neno “kuvyala”- ikimaanisha “kuzaa”, huonekana kwamba si lugha ya upole kuashiria binadamu na yaweza kuleta fadhaa. Neno “kuvyala” likitumiwa kwa mnyama huwa haliathiri uso. Kutokana na utafiti, mtafiti alipata maneno ya Warabai ya kuzungumzia tendo la kuzaa.

### **Miiko ya kuzaa ya Waswahili**

<b>Miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kuzaa	Kuvyaa
Kuavya	Kuharibu mimba
	Kuharibika mimba kimakusudi

Hii yaonyesha kwamba Waswahili hutumia tasfida nyingi wazungumzapo juu ya mambo ya uzazi.

### **Miiko ya kuzaa ya Warabai**

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kuvyala	Kuzaa

<b>Tasfida</b>	<b>Maelezo</b>
Kupata mwana	Kupata mtoto
Kudzifugula	Kujifungua
Kugavya maroho	Kugawanya roho/uhai
Kuhewa mwana	Kupatiwa mtoto
Kumvunguka	Kupangua

#### **3.2.3 Msamiati wa kubaka**

Kubaka ni kitendo cha kulazimisha cha ngono, kitendwacho na mtu asiyehusiana na muathiriwa, au rafiki. Ni kitendo cha nguvu nyingi kinachohusiana na ngono. Katika jamiii ya Warabai kubaka hakutokei kwa watu waliooana. Kwani umuhimu wa kuo ni kufanya ngono. Kwa hivyo mabibi hawawezi kubakwa na bwana zao. Kubaka katika Warabai ni tendo la wanaume watu wazima na wasichana wadogo ambao hawawezi

kujiamulia kufanya ngono au la. Kwa hivyo katika jamii ya Warabai, hii huitwa “kumuminya mhoho”, kumaanisha kumshika msichana kwa lazima. Pia wanawake watu wazima hubakwa na vijana.

“Kumuminya mhoho au mtu mzima” ni msemo wa tasfida kwa sababu hausemi wazi ni nini. Pia watu wazima, kwa sababu fulani hubaka watu wazima wenzao kwa sababu ya kutoweza kujizuia. Pia husemekana na kuaminika kwamba mtu akiwa na Ukimwi akimbaka msichana bikira hupona Ukimwi. Katika hali hii, huwa ni ubakaji lakini huchukuliwa kuwa ubakaji kama muathiriwa atalalamika. Hii huchukuliwa kama kulima shamba la mwenyewe bila idhini.

### **Jedwali 3.2.3 Warabai**

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kubaka	Kuminya

<b>Maneno ya miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kumuminya msichana	Kumshika msichana kwa lazima
Kumhomba kwa lazima	Kufanya ngono kwa lazima
Kumgwira umiro	Kumshika msichana koo
Kumlinga ndore	Kumwangusha

### **Miiko ya kubaka ya Waswahili**

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kubaka	Anamuharibu,kumuingilia mwanamke kwa nguvu
Kulawiti	Kumdanganya ,kuingilia mwanamume

Hii yaonyesha matumizi ya tasfida kuhusu mambo ya ubakaji kama vile Warabai.

### **3.2.4 Hedhi**

Allan na Burridge (2006:144), wanasema kuna uhusiano baina ya mambo ya uchawi na uchafu unaotoka mwilini mwa binadamu. Wanasema kwamba uhusishaji na vitendo si ushamba pekee bali ni vitendo vya karne ya ishirini na moja. Kwa mfano, katika tamaduni nyingi, Warabai wakiwa wamoja wao, kuna masharti ya vile wanawake wana uwezo wa kutumia matendo ya miiko ya uchafu utokao mwilini kama vile damu ya hedhi kuvutia wanaume kingono kwa kuwatilia wanaume kwenye vyakula vyao au vinywaji.

Lengo letu hapa ni kueleza maneno ya miiko na tasfida juu ya uchafu utokao mwilini mwa mwanamke, hasa hedhi katika jamii ya Warabai. Kuna matendo mengi ya mwili ambayo husababisha kutokwa na vitu mwilini. Imani za Warabai husababisha watu kuchukulia mambo haya kwa viwango tofauti vya kuudhi. Yafuatayo ni mazungumzo juu ya aina nyingi ya majimaji yatokayo mwilini mwa mwanadamu hususan mwanamke.

Hedhi hutokea baada ya muda wa siku ishirini na nane za kila mwezi. Yai la uzazi hutolewa mara moja wakati wa kabla hedhi kuwa tayari kwa utungisho wa mimba. Kama yai halitatungishwa mimba, damu inayojenga ukuta wa mji wa mimba hutoka kuitopia uke wa mwanamke. Hali hii huwa yaudhi na watu wengi hutumia vitu kuzuia kutapaka kwa hedhi. Damu hii ikionekana na watu hadharani, huleta aibu kwa mhusika na huonekana kama mwanamke asiyе mwangalifu. Hili ni jambo la kutishia uso. Binadamu wametamaushwa na jambo la hedhi tokea zama za kale.

Kwa upande mwingine, kuna imani kwamba wanawake wanapokuwa kwenye hedhi huwa wachafu na huhatarisha maisha yao na ya wengine. Na upande mwingine yahusiana na uwezo wa kushika mimba na maisha yenyewe, na kwa hivyo huonekana kama jambo muhimu la mwili.

Mtafiti aligundua kwamba ni jambo la hatari katika Warabai na mwiko kufanya ngono na mwanamke aliye kwenye hedhi na angeweza kudhurika. Warabai waabuduo dini ya kienyeji hedhi ni mwiko kufanya hivyo.

Utakuta wasichana wakipenda kula maembe mabichi.

Wanawake walio kwenye hedhi hushauriwa wawe safi,

Kuna maneno yatumiwayo na Warabai juu ya miiko ya hedhi.

### **Jedwali 3.2.4 Warabai**

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kuvudza	Kujuja

<b>Maneno ya miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kuona mwezi	Kuona mwezi
Mwezini	Mwezini
Ajeni	Wageni
Kulumwa ni ndani	Kuumwa na tumbo
Muruo	Kutoka damu nyingi
Kukala mche	Kua mke

Misemo iliyotumiwa ni ya upole, bila kutishia wasichana wadogo kwa yale yawangojeayo mbeleni, katika hali yao ya hedhi.

Mtafiti aligundua kwamba tasfidazingine ni za kihistoria, kabla kuja kwa visodo, wasichana walikuwa wakitumia matambara, lakini kwa sababu za mabadiliko ya kiteknolojia ambazo zimeleta visodo, dhana ya matambara hutumiwa kama tasfida ya muda mwanamke akiwa mwezini.

Mtafiti pia aligundua maneno mengine hutumiwa waziwazi na wazungumzaji. Kwa sababu humaanisha kinachotajwa. Kwa mfano, kama mwanamke akisema, "naombola mlatso", akimaanisha anatoka damu, hili ni jambo ambalo latukia. Pia aligundua kwamba tasfida itumikayo ya hedhi kama vile, "kona" kumaanisha kuona wamezoea kuyasikia, na mhusika hayachukuliwi kama tasfida tena. Kijumla, tasfida za hedhi hutumika kwa sababu wanawake wengi hawapendezewi na kusema wazi juu ya mambo ya hedhi. Wanawake wa Kirabai wawapo katika hedhi, hutumia neno la tasfida kama "ni mkongo" yaani ni mgonjwa ili wasiwaudhi waume zao. Kutokana na utafiti, mtafiti aligundua kuwa wake kwa waume hawafurahii mambo yahusuyo hedhi. Waswahili husema yuko mwezini.

### **Hedhi Waswahili**

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Hedhi	Hoidhwi. Mwanamke kupata hali yake ya kawaida (siku saba)
Hedhi	Ada ya mwezi

Jedwali hili laonyesha Waswahili wakiheshimu miiko ya hedhi kiasi cha kuwafanya kutumia mikakati kutajia mambo haya.

### **3.2.5. Kunya**

Hii ni hali ya mtu au binadamu kutoa uchafu kupitia tundu iliyoko mwisho mwa utumbo mkubwa. Jambo hili huchukuliwa na Warabai kuwa chafu, ambalo hutendwa pahali maalumu “dzalani” ikimaanisha chooni, katika hali ya upole. Neno chooni huepukwa kwa vile huchukuliwa kwamba latishia uso na badala yake mtu husema “nenda nikadzisaidie.” Ikimaanisha kwenda kujisaidia.

Sana sana Warabai hujisaidia kwenye kichaka au msituni. Ni mwiko kwa Warabai hasa watu wazima kujisaidia ndani ya nyumba au mlangoni pa nyumba. Pia ni mwiko kunya kwenye maji au mtoni. Maneno haya yaonyesha kwamba Warabai ni wastaarabu hawanyi ovyo ovyo. Kunayo maneno ya tasfida yatumiwayo na Warabai kuhusiana na kwenda chooni au kunya.

#### **Jedwali 3.2.5 Warabai**

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kunya	Kunya
Mavi	Mavi, kinyesi

<b>Maneno ya miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kwenda haja	Kwenda haja
Kwenda haja bomu	Kwenda haja kubwa
Kupigatsi	Kukojoa
Kudzisaidia	Kujisaidia

Warabai, kwa sababu ya hisia kali juu ya kinyesi, huchukulia uondowaji wa kinyezi kwenye sehemu ya kutolea kinyesi kwa kupafuta kwa kutumia marifu (sehemu ya juu ya

maganda ya nazi), majani ya miti, na pia kuzhondoha (kuburuta makalio kwenye mchanga) ili kundoa kinyesi. Siku hizi, kwa sababu ya utamaduni wa kisasa, Warabai wengi hutumia maji kunawa, ingawaje wengine bado wanatumia majani ya miti.

Kutokana na tasfida za Warabai kuhusiana na kunya, lugha ya Kirabai yajaribu kutumia upole katika maneno ya miiko ya kunya kwa kutumia maneno kama, “kudzisaidia.” Jedwali la kunya ya Waswahili.

#### **Jedwali la mwiko wa kunya ya Waswahili.**

Mwiko	Maelezo
Kunya	Kunya
Kunya	Kuenda haja kubwa

#### **3.2.6. Kukojoa**

Mkojo ni majimaji ya manjano yatokanayo na mchujo wa maji ya chujwayo na figo. Hili ni jambo muhimu mwilini.

Mtafiti aligundua kwamba kukojoa si jambo ambalo laweza kuongewa ovyo ovyo, hususan katika hali ya upole, na kama mtu yambidi kulisema, basi angetumia maneno ya tasfida kutajia ili asiwafanye watu kutahayari. Katika tamadauni nyingi Warabai wakiwa mojawapo, wanaume hukojoa wakiwa wamechuchumaa na wanawake vile vile huchuchumaa. Hakuna tofauti baina ya vile wanaume hukojoa na wanawake. Hii hufanyika pahali pa siri si hadharani, kwa vile kukojoa huchukuliwa kama jambo la kutisha uso.

### **Jedwali 3.2.6**

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kukodzola	Kukojoa

<b>Maneno ya miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Haja tite	Haja ndogo
Kupigatsi	Kupiga nchi
Kutsuya mahe	Kutema mate
Kujisaidia	Kujisaidia

### **Jedwali la mwiko wa kukojoa wa Waswahili.**

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kukojoa	Kukojoa
Kukojoa	Haja ndogo

Mtafiti aligundua kwamba, Warabai huchukulia jambo hili kuwa nyeti na ambalo huweza kuleta laana kwa mtoto kumuona mzazi wake akijisaidia, hasa akiona sehemu za babake au mamake za siri. Hii ndio sababu Warabai hujisaidia mahali siri ni kama vile bomani (uwa ambalo hujengwa na majani ya mnazi) au hujificha kichakani wakiangalia huko na kule kabla kukojoa.

### **3.2.7 Mwiko wa Kifo**

Kuwasilisha, kufasili, kufafanua miiko na tasfida ya kifo. Kifo ni jambo ambalo laogofya na halizoleki na mwanadamu yejote au hata viumbe wengine wenye uhai. Warabai wanaogopa kifo sana na wana kisa asili cha kifo. Inasemekana Mrabai wa kwanza aliishi na mkewe kwa raha na starehe, lakini siku moja, baada ya kupata watoto wa kike na wa kiume, alipatwa na ugonjwa na akafa.

Kwa vile lilikuwa tukio la kwanza alishtuka. Akawaambia wanawe ambao walimshauri wakakitafute kile kifo. Walikitafuta lakini hawakukipata. Wakaazimia kutafuta njia ya kukitupa. Hapo basi iliamuliwa kwamba mtu afiliwapo na bibi au bwana, lazima atafute mtu ambaye si Mrabai alale naye mara moja wala asimrudie tena. Hapo basi atakuwa amekitupa kifo kile. Lakini mtu wa kwanza kutupa kifo alifanya makosa kwani alimuelekeza yule aliyetupa kifo naye, na huyu mtu akamfuata. Ingawaje hakulala naye tena lakini kule kuja katika kile kijiji basi, kulifanya kifo kirudi. Na hii ndio imani ambayo imewafanya Warabai wafe. Na kila mtu afapo, basi, kifo hutupwa lakini charudi tena kila wakati. Kwa vile kifo chatisha na hakiepukiki, ni mwiko kwa jamii kukitaja ovyo ovyo.

Hii ni kwa sababu kifo huibua hofu na hisia nyingi kinapotajwa. Kwa sababu kifo hutishiauso wa mwathiriwa, Warabai wanayo maneno ya tasfida ya kutajia kifo mbadala ya lile neno kifo ili kuokoa uso.

Warabai badala ya kusema mtu amekufa, husema “mtu fulani yuhuricha” yaani “mtu fulani ametuacha” kwa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu ya kupunguza makali ya hisia ziletwazo na kifo, kwa kutumia lugha ya upole.

Jedwali hili laonyesha mwiko wa kifo wa Warabai na mikakati iliyodhihirishwa nayo katika matumizi ya kimuktadha.

### **Warabai**

<b>Maneno ya miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kubwewa	Kumeangukwa
Viricha	Vimeacha
Mwongo wehu <u>yuvola</u>	Mgonjwa wetu amepona
Ukongo kaukamtivya	Ugonjwa haukupona
Yudzefa na kusoheka kifo	Amekufa na ugonjwa wa kutoweza kupumua

<b>Chifo</b>	<b>Kifo</b>
Kubanangikwa ni mtu	Kumeharibikiwa na mtu
Kudzasema chifo	Nimekujasema kifo
Yudzefa	Amekufa
Hurichwa	Tumewachwa
Hufererwa	Tumefiliwa

Warabai wanaogopa kifo, lakini hawaogopi maiti. Mtu afapo watu huitwa wamnyoe nywele za kichwani na za sehemu ya siri. Warabai huita mtu aliyekufa, ‘mtu wa kufa au lufu’ hii ni lugha ya upole ya kupunguza vitishio vyatuo kwa kutumia maneno ya tasfida. Kama mtu amekufa, watu husema “Yuhuricha”, kumaanisha amewaaacha jamii

zake.Tasfida za hapo juu zaonyesha upole ni muhimu tunapoashiria mtu aliyekufa katika jamii ya Warabai.

### **Kifo cha kawaida**

Kifo cha kawaida ni pale mtu huacha kuishi. Ingawaje ni jambo gumu, lakini kawaida hukubalika bila maswali mengi na Warabai hupenda kutumia tasfida kwacho.

Mwiko	Maelezo
Chifo	Kifo

Maneno ya miiko	Maelezo
Yuyirika chiko	Amepeleka kiko
Yukwenda lola chinemi	Ameenda angalia mvua[mzizimo]
Yukwenda oya	Ameenda pumzika
Yukwenda mbere za hachi	Ameenda mbele za haki

### **Miiko ya kifo ya Waswahili**

Mwiko	Maelezo
Kufa	Atuatha,ameacha dunia
Kufa	Mwenyezi Mungu amekhitari (Kiarabu)
Kufa	Anfariki, amekufa

**Jedwali hili laonyesha Waswahili watumiavyo mikakati watajapo kifo.**

### **Uuwaji wa binadamu**

Uuwaji wahusiana na kutoa uhai wa binadamu na mtu mwengine.

Katika Warabai mtu auapo mwingine hutozwa malipo. Hii ni kwa sababu mtu mwingine asirudie kitendo kama kile cha kufadhaisha watu.

Yako maneno ya tasfida kwa kitendo hiki kama vile

<b>Maneno ya miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Yutsinza muyawe	Amechinja mwenzake
Yukotwa	Ameapurwa
Yuvirikwa kwa amvuye	Amepelekwa kwa mjombake

### **Kifo kupitia ajali**

Kifo cha ajali chahusisha kifo cha mtu ambacho si cha kawaida. Chaonekana kuwa cha ghafla. Sana sana watu hukihusisha na uchawi au laana.

Miili yao huzikwa mbali ma wale waliokufa kwa magonjwa. Inasemekana kuwa hawa ni ‘watu wa vita’ ndiposa wanatengwa na watu wengine kuepukana na walio hai wasije wakapata ajali pia.

<b>Maneno ya miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Yugongwa na gari	Amegongwa na gari
Yulumwa ni nyoka	Amekufa kwa kuumwa na nyoka
Yudzefa kwa kubwa mnazini	Amekufa kwa kuanguka kutoka kwa mnazi.

### **Kujiuia**

Kifo hiki hutokea kwa mtu kujitoa uhai mwenyewe. Warabai huhusisha aina hii ya kifo na uchawi. Kifo hiki husababisha hofu nyingi kwa walioachwa wakiwa wanaojaribu kutafuta sababu zake na maneno yafuatayo hutumiwa kuelezea aina hii ya kifo.

Mwiko / Tasfida	Maelezo
Yudzidzulaga	Amejiua
Yudzifunga lugwe	Amejifunga kamba
Yudzerya sumu	Amekula sumu
Yudzidzibuma madzini	Amejitia majini / mtoni

Tasfida tulizogundua juu ya mwiko wa kujiua zaonyesha kwamba mtu anayejiua huwa amekusudia. Mifano ya tasfida zitumiwazo na Warabai huziba kifo ili kupunguza hisia za walioachwa.

### **Warabai hufananisha kifo na safari.**

Tasfida zitumiwazo na Warabai ni:

Tasfida	Maelezo
Yukwenda mbere za haki	Ameenda mbele za haki
Yudzenda kuzimu	Ameenda kuzimu
Yudzenda jongomeo	Ameenda jongomeo
Wahuricha	Alituacha tena
Kayo kahiri	Hayuko tena

Mtu afapo husemekana ametuacha, na ameenda

Kutoka katika maisha hadi kifo huonekana kama safari isiyopekwa, na kila mtu ni lazima impate, matumizi ya msemo huu hupunguza tisho la kutaja kifo.

Pia watu hufananisha kifo na kulala.

Tasfida	Maelezo
Yurere	Amelala
Yufinya matso	Amefunga macho

Mtafiti aligundua kuwa athari za kifo hupunguzwa kwa kutumia neno “kulala”. Kwa hivyo tukio la kifo hupunguzwa ukali au uzito kwa kubadilishwa na msemo “kulala”, na “kufunga macho”. Kwa hivyo kifo chaogofya, wana tasfida za sitiari za kifo ili kupunguza hisia za kifo. Kwa hivyo, maneno ya tasfida hutumika badala ya kifo na kufanya kifo kivumilike.

### **3.2.8 Miiko ya Magonjwa –Ukimwi**

Warabai huamini kwamba kifo husababishwa na ugonjwa au magonjwa.Utamsikia mzee wa Kirabai akisema, “nzala kayulaga, uulagao ni ukongo”, yaani njaa haiuwi bali ugonjwa ndio huua.

Kwa hivyo hapa tutachunguza tasfida zitumikazo kuashiria ugonjwa. Magonjwa, kwa upana yaweza kufafanuliwa kama maradhi au unyonge unaoathiri hali ya kawaida ya mwili. Kutokana na utafiti, mtafiti alipata kuwa jamii ya Warabai wanachukulia kuwa magonjwa husababishwa na laana, mashetani au uchawi. Magonjwa yanapozidi watu huhama na kwenda kuishi mahali kwingine “kugaluza pyeho”, kugeuza mazingira ili kuepuka maradhi. Tishio la uchawi limewafanya Warabai kuhama makwao na kuenda kuishi sehemu zingine. Yafuatayo ni maelezo ya maradhi katika Warabai na maneno ya tasfida ya maradhi hususani Ukimwi.

### **3.2.9 Ukimwi**

Ukimwi maana yake ni ukosefu wa kinga mwilini, ambapo mwili huwa katika hatari ya kupatwa na maradhi mbalimbali yatokeapo, na kupelekea mwathiriwa kuaga dunia. Hii ndiyo sababu ya Ukimwi kuogopewa na kupewa majina ya kutisha.

Haya ni maradhi yanayoenezwa kuititia ngono na pia kutumia sindano na vijembe na mtu aliyeambukizwa. Kisa cha kwanza kiligunduliwa nchini Kenya mnamo mwaka wa elfu moja mia tisa themanini na nne na hata waleo hauna tiba. Ukimwi hauna tiba.

Simon (2007), akimnukuu Tessa (2006), katika utafiti juu ya Ukimwi na lugha za Kiafrika, aligundua kwamba Ukimwi ni mwiko wa kisasa. Kuzuka kwa janga hili kumeibua ubunifu wa maneno ya hali jamii zilijaribu kukubaliana na tishio la Ukimwi. Mtafiti aligundua kuwa Warabai hupata maneno ya tasfida ya Ukimwi kutokana na matumizi ya lugha ya kawaida. Mtafiti aligindua kati ya maneno ya mwanzo mwanzo ya tasfida ya Ukimwi ni neno “*gwangula*”, kumaanisha ugonjwa wa ngozi wa kujikuna mwili mzima. Kwani mtu wa Ukimwi mwili wake hupatwa na ugonjwa wa ngozi, na vidonda mwili mzima na majipu. Kwa hivyo jina hili linaashiria madhara ya kuambukizwa Ukimwi. Neno hili, “*gwangula*” lilileta fedheha kwa mwathiriwa wa Ukimwi.

Na jina hili la Ukimwi lilitumiwa kuonya dhidi ya kuambukizwa maradhi haya yaliyohusishwa na kufanya ngono bila kinga au hata watu waendapo kwa waganga na kuchanjwa kwa kutumia wembe mmoja na iwepo kwamba mmoja wao ni mwathiriwa.

Mtafiti aligundua kwamba maneno au majina mengi ya Ukimwi yalibuniwa baada ya kuibuka ugonjwa wa Ukimwi ili kuonyesha vile ugonjwa huu ni hatari. Na hii haikupeana matumaini kwa wale waliokuwa wameambukizwa. Hii ilifanya watu wote kuogopa ugonjwa wa Ukimwi. Hii ni kwa sababu Ukimwi hauna tiba na hupelekea mauti kwa mtu apatwaye nao. Maneno ya tasfida ya kutajia mwiko huu wa Ukimwi ni yafuatayo.

<b>Neno la tasfida</b>	<b>Maelezo yake</b>
Ukongo wa UKIMWI	Ugonjwa wa UKIMWI
Unahiwa tego	Unaitwa kaswende
Wabwirwa ni spaki Yuna spaki	Alishikwa na spaki ana spaki
Ukongo wa dzenya kare	Ugonjwa wa nimekunya tayari
Ukongo wa kufyoka na <u>kuvavika</u>	Ugonjwa wa kuhara na kutapika
Ukambi	Ukambi
Ukongo wa nyerenyere	Ugonjwa wa udhaifu
Baha dzana	Afadhal jana
Ukongo wa chisambi	Ugonjwa wa kisasa
Ukongo uriokudza	Ugonjwa uliokuja
Ukongo mubomu	Ugonjwa mkubwa
Walumwa ni kabuzi	Aliumwa na mbuzi
Umeme	Umeme

### **Miiko ya Ukimwi ya Waswahili**

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Ukimwi	Ukimwi
Ukimwi	Umeme
Ukimwi	Ngoma

Hii yaonyesha kwamba Waswahili hawatumii tasfida juu ya ugonjwa wa Ukimwi kuliko Warabai. Maneno haya yaliyotajwa yatishia uso, haswa kwa mwathiriwa anayeugua Ukimwi. Hayatilii maanani mahitaji ya uso wa muathiriwa wa Ukimwi. Hii inamaanisha kwamba ingawaje yatumika kama maneno ya tasfida yanaegemea upande mmoja. Mtafiti aligundua kwamba baada ya muda wa kugunduliwa kwa Ukimwi, unyanyapaa umeendelea kupungua na maneno ya upole yalibuniwa katika lugha ya Kirabai ambayo yalikuwa ya upole na yaliyopunguza vitishio vya uso.

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Gwangula	Ukimwi

<b>Tasfida</b>	<b>Maelezo</b>
Homa	Mafua

Majina haya ya Ukimwi hupunguza hisia yakilinganishwa na ya awali kwa matumizi ya neno “homa” kuashiria kwamba si jambo kubwa na huonekana kuwa sawa na magonjwa mengine. Maneno haya ya tasfida hutumiwa kuondoa hofu na shutuma. Ukimwi huonekana kama “ajali” maana mtu yejote huweza kuambukizwa Ukimwi. Kwa hivyo, si ugonjwa uhusianao na uzinzi au uasherati tu. Watu wanapozungumzia ugonjwa wa Ukimwi kama “gwangula”, kwa kutaja Ukimwi, vijana walioelimika hutumia maneno ya kiteknolojia kutoka Kiingereza kama kutumia neno “yuna spaki”. Hili ni neno mkopo kutoka Kiingereza. Watu wazima hutumia neno “walumwa ni mbuzi”, kumaanisha kutahadharisha kwamba huleta unyanyapaa na watu wastahili kuepuka kufanya ngono bila kinga.

### **3.2.10 Miiko na Tasfida ya Kubaleghe ya Warabai**

Kubaleghe ni hali ya kutoka utotoni hadi utu uzima. Hili ni jambo la kimaumbile ambalo kila mtu humpitia. Jambo hili huambatana na mabadiliko ya kiviungo, tabia na hisia. Ni jambo litokalo na lihitajilo kupewa heshima kubwa. Mtu aliyeboleghe huhitaji kupewa heshima kubwa. Huwa ni mtu aliyejigutukia mambo yanambadilikia. Hii huambatana na sehemu nyeti kugeuka. Mvulana sauti yake hugeuka kuwa nzito, humea nywele usoni au ndevu, humea nywele makwapani na sehemu za siri. Msichana naye sauti yake hugeuka na kuwa nyororo. Humea nywele makwapani, humea nywele sehemu za siri na vile vile huota matiti. Vitu ambavyo huwfanya kuwa na haya yingi, na wenye hisia nyingi.

Huvutiwa na watu wa jinsia tofauti na yao. Hii ndio sababu kukahitajika mikakati ya kupunguza au kuepuka tataruki ziletwazo na kutajwa mambo ya kubaleghe ovyo ovyo. Hii ndio ilipelekea utumizi wa maneno ya tasfida yatumikayo badala ya yale ya miiko. Kwa hivyo tulichunguza semi za tasfida za kubaleghe za Warabai tukitumia nadharia za upole. Zifuatazo ni tasfida ya maneno ya patikanayo katika watumizi lugha ya Kirabai. Jedwali lifuatalo laonyesha miiko na tasfida ya kubaleghe ya Warabai.

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kubaleghe	Kubaleghe

<b>Tasfida</b>	<b>Maelezo</b>
Kubaleghe	Kubaleghe
Kukala mtu mzima	Kuwa mtu mzima
Kuvunza ungo	Kuvunja ungo
Yukala mlume	Amekuwa mume
Yukala mche	Amekuwa mke

Mwana yudzaluka	Amechana kama maua
Yukala wa mche	Amekuwa wa mke
Yukala msichana	Amekuwa msichana
Yufika wa kuhalwa	Amekuwa wa kuolewa
Yufika wa mche	Amefika wa mke
Yuvunza umiro	Amevunja sauti
Yufika wa kuhala	Amefika wa kuoaa

### **Miiko ya Kubaleghe ya Waswahili**

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kubaleghe	Kuvunda ungo - miaka tisa hadi kumi na miwili

Waswahili hawana utumizi wa tasfida waongeapo juu ya kubalekhe.

Kulingana na utafiti wetu tumegundua kwamba miiko na tasfida ya kubaleghe ya Warabai ina semi nyingi zinazozingatia mikakati ya upole.

Kwa mfano Warabai wakitaka kusema mvulana amebaleghe husema, “yuvunza ungo”, humaanisha amebadilika kimaumbile katika Kiswahili. Hii ni hali ya kutumia lugha kistaarabu ili kutokera watu au kuwavunja watu heshima, kwani mambo ya kubaleghe ni mambo nyeti hayatamkwi ovyo ovyo. Pia Warabai hutumia lugha katika mikakati ya kupunguza ukali. Hii yote ni kuleta kudumisha heshima kwa kutumia maneno mbadala ya yale ya miiko. Hii imewiana na nadharia ya upole tulioitumia.

### **3.3 Miiko ya Vyakula visivyoliwa na Warabai**

Chakula ni kitu muhimu kwa mwanadamu. Hii ni kwa sababu humsaidia mtu kuwa na afya nzuri, humpa nguvu za kupambana na maradhi, pia humpa afueni ya haraka anapouga maradhi. Lakini si vyakula vyote huliwa na kila mtu. Kwa hivyo, tulitafiti kuhusu vyakula ambavyo Warabai hawali. Hii ni kwa sababu za mila na desturi na hata sababuza kidini kwamba walapo watadhurika na hata kuwa wagonjwa.

#### **Jedwali laonyesha vyakula ambavyo Warabai hawali.**

Miiko	Maelezo
Chakurya	Chakula

Maneno ya miiko	Maelezo
Mfu	Mnyama aliyekufa mwenyewe
Chisonya cha miya	Mchicha mwitu
Munyu mtu achikala na pyeho	Chumvi mtu akiwa na kiharusi.
Uchi uriobumwa maji	Tembo la mnazi lililotiwa maji
Chakurya cha mafuha	Chakula kilichopikwa kwa mafuta.
Chakurya chidzicho jitwa ni mtu ariye mwezini	Chakula kilicho pikwa na mtu aliye kwenye hedhi.
Logatsi	Logatsi
Tsalakushe	Mboga mwitu
Lwenza lwa mnazi	Ncha ya mnazi
Matoke	Matoke
Muthokhoi	Mahindi na maharagwe

Mtafiti aligundua kwamba kuna vyakula vingi ambavyo Warabai hawali, kwa sababu ya kukatazwa na mila na desturi zao. Warabai hawali mnyama aliyekufa mwenyewe hakuchinjwa. Hii dhana imeletwa na athari za dini ya Kiislamu ambayo yakataza mtu asile nyama ya mnyama ambaye hakuchinjwa na Mwislamu kwa kusomewa dua kabla ya kuchinjwa. Hii ni kwa sababu Warabai wengine ni Waislamu. Tasfida ya miiko hii imeambatana na nadharia ya upole.

### **Jedwali la vyakula visivyoliwa na Waswahili.**

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Vyakula visivyoliwa	Vyakula visivyoliwa
Vyakula visivyoliwa	Muhogo wa mpira

#### **3.3.1 Miiko na Tasfida ya Wanyama Wasioliwa**

Wanyama wachinjwapo na kupikwa huwa chakula cha binadamu chenye madini yenye kujenga mwili na kuulinda dhidi ya maradhi, lakini si wanyama wote huliwa, kwani wengine waliwapo huweza kuleta madhara na hata ugonjwa – kama vile ngozi, kujikuna kuna. Pia wanyama wengine, jamii fulani zimekatazwa kuliwa kulingana na imani zao za kidini. Kwa mfano, Warabai, hawali mnyama wa nyasini – yaani nyoka.

<b>Miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Mnyama	Kiumbe ambaye si binadamu
Mnyama wa nyasini	Nyoka
Tsimba	Simba
Tsui	Chui
Fisi	Fisi
Ng'onzi	Kondoo
Kuye	Panyabuku
Mwee	Mwewe
Gungu	Kunguru
Mabeshe	Samaki

Tsomvi	Mtonzi
Mbuta	Mbuta
Kobe zia	Kasa
Paka	Paka
Kobe	Kobe
Kola	Konokono
Tsongo aryaye nyama	Ndege alaye nyama.

### **Wanyama wasioliwa na Waswahili**

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Nyoka	Adui ,mdudu mnyama wa nyasini (kutokana na hadithi ya Quran)
Kunguru	Ndege alaye nyama
Nguruwe	Nguruwe ,mnyama najisi
Tai	Ndege alaye nyama
Simba	Mnyama mla nyama
Chui	Thui mnyama mla nyama
Paka	Mnyama ala nyama aishie nyumbani.
Mbwa	Kuro,mnyama najisi

Na wengeni, kama kiboko, ndovu, pundamilia, mbweha, twiga, panya, mamba, ndege wenye makucha, na kobe.

#### **Jedwali laonyesha wanyama wasioliwa na Waswahili.**

Tulithibitisha kwamba kuna tasfida juu ya miiko ya wanyama wasioliwa na Warabai. Kila neno la mwiko wa wanyama wasioliwa lina neno mbadala yake la tasfida ingawaje mengine hayana majina ya tasfida kama vile kobe, fisi na paka.

#### **3.3.2 Miiko na Tasfida ya Ndoa**

Ndoa inamaanisha watu wawili wa jinsia tofauti, yaani mke na mume wanapoungana na kuwa mke na mume. Hivi karibuni kumekuwa na ndoa za watu wa jinsia moja, mume

kwa mume, mke kwa mke, hususani kule magharibi ya; Marekani. Hii ni kwa sababu madhumuni ya watu kuoana wafikapo umri wa kufanya hivyo ni kupata watoto. Hii haiwezekani pale watu wa jinsia moja waoanapo.

Warabai wanapinga ndoa za watu wa jinsia moja na hata ngono ya watu wa jinsia moja. Watu wafanyapo mapenzi wakiwa wa jinsia moja hubidi kutolewa kafara, kondoo achinjwe. Mtu atakapofika umri wa kuoa, wazazi humtafutia mke na kumtolea mahari. Mwisho basi huweza kuunganishwa na kuwa mke na mume.

Ndoa ni jambo lihitajilo heshima maana lafungamana na masuala nyeti katika jamii. Maana ya fungamana na ngono, ambalo ni jambo linaloheshimiwa. Kwa hivyo, ndoa haitajwi ovyo ovyo, ndio sababu kunayo maneno mbadala ya tasfida yanayotumiwa na Warabai. Jedwali lifuatalo laonyesha misemo ya miiko na tasfida itumiwayo na jamii lugha ya Warabai.

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Nyambura	Ndoa

<b>Tasfida</b>	<b>Maelezo</b>
Ndoa	Mume na mke wanapooana.
Kupata dziko	Kupata jiko
Wapata muyawe	Alipata mwenzake
Wahala	Alioa.
Waiya mche	Aliiba mke.
Wasukumirwa	Aliozwa kwa lazima.

Warabai hutumia maneno ya tasfida ya upole ili kuepuka kutishia uso. Hii ni mikakati ya upole ya kuokoa uso wa muhusika. Hii yaonyesha kwamba Warabai hutumia maneno ya tasfida mbadala ya yale ya miiko ili kudumisha heshima –maana maneno ya miiko kutaja bure bure ni mwiko.

### **Miiko ya ndoa ya Waswahili (Wajomvu)**

<b>Tasfida</b>	<b>Maelezo</b>
Ndoa	Mikaha, kuleta Kadhi kufunganisha watu
	Walii–kukubali kwa mzazi wa kiume mtoto aolewe na mtu fulani.

### **Miiko na tasfida ya kifo ya Waswahili –Wajomvu**

#### **Jedwali**

<b>Maneno ya miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kufa	Anfariki, kaaga dunia
<b>Tasfida</b>	<b>Maelezo</b>
Aga dunia	Amekufa
kufiliwa	Kumekufa mtu
kupotelewa	Kumefiwa
Amalizika	Amekufa
Mungu amemuhitaji	Amekufa
Ankufa	Amekufa
Mnitari	Maiti

Hapa tuliona kwamba kuna kulingana kwa baadhi ya maneno yatajayo kifo. Warabai husema “yudzefa” yaani amekufa na Wajomvi nao husema “ankufa” yaani amekufa. Wajomvi husema “amekufa” ambayo ni sawa na husema “yudzefa” kwa Kirabai.

Jedwali la miiko na Tafsida ya ukimwi ya Waswahili.

### **3.4 Hitimisho**

Katika sura hii, tumeweza kuwasilisha na kuchambua data tuliokusanya kwa kupitia mahojiano, hojaji na hata uchunguzi kwenye matukio halisi ya mazishi na matanga na harusi za wenyiji juu ya miiko na tasfida ya miiko ya Warabai na Waswahili ya ndoa. Tumeweza kuonyesha vile imedhihirisha mikakati ya kimaana katika uelekezi wa nadharia ya upole.

Tumetumia majedwali kuziorodhesha na kuzitafsiri kimatumizi ya Warabai. Kila mwiko umeonyesha mikakati iliyotumika kuielezea kimuktadha. Tumetafsiri kutoka Kirabai hadi Kiswahili sanifu na Kijomvu hadi Kiswahili sanifu. Katika sura hii tumeangazia miiko na tasfida ya Warabai na Wajomvu ifuatayo, kifo, ndoa, maradhi-Ukimwi, kubalehe, kuwa kwenye hedhi, Ngono, Kubaka, Kunya, na Kukojoa.

Kutokana na majadiliano na mifano ya tasfida na miiko tulioangalia katika jamii ya Warabai, inadhihirika wazi kwamba miiko ni mambo ambayo yaheshimiwa sana. Warabai na Wajomvu hutumia lugha kisitiara kuzungumzia mambo nyeti katika jamii kama kifo, ngono, Ukimwi na ndoa. Matumizi ya maneno ya tasfida badala ya yale ya miiko, ni kupunguza athari zinazoashiriwa na miiko husika.

Matumizi ya “homa” ambayo ni mafua kwa ugonjwa unaoua kama vile Ukimwi ni kupunguza tishio la ugonjwa wa Ukimwi. Sio kila mwiko wa Warabai ni mwiko. Kuwa mwiko kwa jambo katika jamiii ya Warabai hutegemea mambo kama umri, uhusiano na wakati maalum. Katika sura ifuatayo tunahitimisha utafiti na vile vile kupeana

mapendekezo ya utafiti juu ya miiko na tasfida ya Warabai-wa wilaya ya Rabai kwa jumla na kulinganisha na ile ya Wajomvu na kutoa maoni juu ya mada.

**SURA YA NNE**  
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **4.1 Utangulizi**

Katika sura hii, tunatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti, mapendekezo ya tafiti nyingine juu ya mada hii ya miiko na tasfida katika jamii ya Warabai na vile vile Wajomvu na kutoa hitimisho la utafiti wetu. Kutokana na utafiti wetu, tumeweza kujadili nadharia tete zetu pamoja na kuangazia matitizo ya utafiti tuliyokumbana nayo.

#### **4.2 Muhtasari na Hitimisho**

##### **Muhtasari wa matokeo**

Lengo kuu la utafiti unahusu misamiati ya miiko na tasfida ya Waswahili na Warabai. Miiko na tasfida yazingatia masuala mbalimbali yanayokatazwa katika jamii. Majukumu yanayotekelawa na miiko na tasfida yazingatia masuala mbalimbali yanayokatazwa katika jamii ingawaje miiko imeshunghulikiwa na watafiti wengi, ile ya Wajomvu na kulinganisha na ile ya Warabai haijashughulikiwa.

Katika utafiti wetu tulilenga kuchunguza malengo yafuatayo: Kutambua na kuelezea miiko na tasfida inayotumiwa sana na jamii lugha ya Warabai na ya Waswahili. Kugundua misemo inayohusishwa na miiko na tasfida ya Warabai na vilevile Waswahili. Kuchunguza umuhimu wa maneno ya tasfida inayotumiwa na jamii lugha ya Warabai na Waswahili.

Sura ya kwanza ya utafiti, ilishughulikia utangulizi, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu ya kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada, na mbinu za utafiti. Sura hii ndiyo ilikuwa msingi wa kazi yetu. Katika sura ya pili, tulishughulikia fasili ya miiko. Tumeweza kueleza miiko ni nini. Tumeangazia kanuni na matumizi ya miiko Warabai, ambapo tumeangazia kanuni za matumizi ya miiko ikiwa ni pamoja na kanuni ya umri ya wanaowasiliana ikiwa ni kama vile watu wazima na watoto.

Pia tumeangalia kanuni za matumizi ya miiko kama vile uhusiano wa mzungumzaji na hadhira yake. Kama vile mtu mzima anavyowasiliana na mkaza mwanawe kwa kutumia tasfida nyingi ya miiko kuliko pale anayezungumza naye akiwa mwenye kuzoeana naye. Pia kuna mikakati ya kimazingira. Utakuta miiko huvunjwa sana kulingana na hadhira na mahali mahususi. Kwa mfano, kwenye maombolezi, uvunjadi wa miiko huwa mwingi sana kuliko katika harusi.

Maneno ya matusi husheheni mazungumzo na nyimbo za maombolezi bila kujali hadhira. Katika sura ya tatu, tulijikita katika uchambuzi wa misamiati ya miiko na majukumu ya miiko yanayojitokeza katika matumizi ya Warabai na Wajomvu. Tumeangalia semi za miiko ya Warabai na Waswahili juu ya maradhi-Ukimwi, kifo, ndoa, ngono, kubaleghe, wanyama wasioliwa, vyakula visivyoliwa, kunya na kukojoa. Utafiti umegundua kwamba maneno ya tasfida katika Warabai na Wajomvu yalizushwa na kuweko kwa miiko. Data ya tasfida ya ngono katika jamii ya Warabai hutumia misemo kama “kumumanya”- kumjua ikimaanisha kufanya ngono.

Inapofika kwenye data ya mambo ya kuwa mwezini, Warabai husema “yuna vudza” yaani anavuja kumaanisha kwamba yuko katika ada ya wanawake kwa njia ya kiheshima na upole.

Utafiti pia uligundua kwamba Warabai hutumia lugha kistiara kuashiria mambo ya miiko na tasfida. Tasfida kama “walumwa ni mbuzi” kumaanisha Ukimwi na “gwangula” yote ni maneno ya tasfida juu ya Ukimwi.

Wanapozungumzia kifo, Warabai hutumia tasfida kama vile, “kwenda lola chinemi” Wajomvu husema amelala huwa ni misemo inayotumiwa kupunguza ukali wa kifo. Kwa kiwango fulani, utafiti umegundua kwamba tasfida katika lugha ya Kirabai hutumiwa kuficha ukweli na kuhalalisha tabia mbaya. Kwa mfano, kubaka msichana mdogo huitwa “kumuminya” yaani kupigana naye.

Misemo mingi hujaribu kuashiria matendo ya ngono kwa njia ya upole kuliko vile yalivyo. Hii ni kama kuficha ukweli wa mambo na kuyafanya kuwa ya kawaida. Kama vile, “kulala na mche wa mtu” yaani kwa Kiswahili sanifu, kulala na mke wa mtu. Kwa kutumia neno, “kulala” hufanya jambo hili kuwa kawaida. Ambapo kulala na mke wa mtu si jambo la kawaida.

Katika hali hii ya mitazamo juu ya kuhalalisha makosa kwa kuficha ukweli, hujaribu kuonyesha aina ya tasfida itumikayo katika Warabai huathiri ukweli na uongo wa vile wanvyoolewa madhumuni yao katika maisha. Kwa mfano neno “wabwirwa ni spaki”

alishikwa na spaki ikimaanisha Ukimwi ikilingwanishwa. Utafiti umegundua kwamba sio maneno yote ya miiko katika jamii ya Warabai bali hutegemea umri, uhusiano, tukio na wakati mahususi. Tumegundua kwa sababu ya kufululiza kwa lugha kumesababisha kuwe na kulingana kwa miiko na tasfida ya Warabai na Waswahili. Hii ni kwa sababu lugha haina mpaka dhahiri.

#### **4.3 Mapendelekekezo**

Utafiti huu ni juu ya miiko na tasfida ya jamii moja ya Waswahili na kulinganisha na ya Warabai kama vile kifo na magonjwa na mengineyo kama mipaka na upeo wa utafiti.

Katika harakati za utafiti, mtafiti aligundua kuna mengi yanayoweza kutafitiwa juu ya mada tulizotafiti kwa hivyo tungeomba kupendekeza tafiti nyingine zifanywe. Kulinganisha miiko na tasfida ya sehemu za siri na maji maji yanayotoka katika mwili kama vile mate najasho ya Warabai na ile ya Waswahili. Tafiti zifanywe juu ya miiko na tasfida ya sehemu za siri za uzazi za uke na uume katika Warabai na Waswahili na kuzilinganisha.

#### **4.4 Hitimisho**

Katika hitimisho, sura hii, tumepeana muhtasari wa matokeo ya utafiti. Nadharia tete ambazo utafiti ulilenga kujaribu au kutumia zimethibitishwa kuwa ni ukweli. Sampuli tuliyotumia ilihusu mambo nyeti katika jamii, ilikuwa vigumu kupata maana si rahisi mtu kuzungumzia mambo nyeti ovyo ovyo. Hii ilifanya ukusanyaji data kuwa na changamoto kubwa sana. Vile vile wanaojua miiko ni watu wazima ambao hawajaathiriwa na usasa, ambapo huwezi kupata watu ambao hawajaathiriwa na usasa katika jamii.

Jambo lingine lilikuwa ukosefu wa fedha za kutosha za kumwezesha mtafiti katika usafiri hadi sehemu ambazo ukusanyaji data ultakikana. Kupata vitabu vinavyohusika na nadharia ilikuwa vigumu kupatikana maktabani kwani ni vichache mno na vilivyoko hususani ni vichache mno na vingi viko katika lugha ya Kingereza.

Mwisho, muda wa utafiti ulikuwa mfupi kuweza kupata habari nyingi zilizotakikana. Changamoto tulizozipata gharama za utafiti za pesa, kupata wa tafitiwa wenyekujua yafitiwayo haikua rahisi eneo la utafiti lilikuwa kubwa mno, ni badhi tu ya changamoto tulizokumbana nazo katika utafiti. Uvunjaji mwingi wa miiko ulipatikana katika maombolezi ya Wirabai ambapo siku hizi nyimbo zinazotumiwa kwenye maombolezi si za Kirabai kwa sababu ya dini za Kikristo na Kiislamu. Licha ya changamoto hizo, tuliweza kukusanya data ya kutosha iliyotufaa katika utafiti wetu.

## MAREJELEO

- Allan, K. and K. Burridge (2006). *Forbidden Words. Taboo and the Censoring of Language*. Cambridge. Cambridge University Press.
- (1991). *Euphemism and Dysphemism*:New York: Oxford University Press.
- (1991). *Euphemism and Dysphemism: Language Used as a Shield and Weapon*.New York: Oxford University Press.
- Bonvillan, J.D. (1997). *Theoretical Approaches to language Acquisition*. In J.B. Gleason (ed) the Development of Language (4<sup>th</sup> edition) Boston: Allyn and Bacon.
- Brown P. na C. Levinson (1976). *Universal in Language Usage*: Politeness phenomena, Cambridge .Cambridge University Press.
- Evans, R. and Velde Peterson (2000). *Taboo Topics*. New York: Atherton press, 8-21.
- Fair, L. (2001 ). *Pastimes and politics culture, community and identity in post-Abolition urban Zanzibar, 1890-1945*: Ohio University Press.
- Firth, J. (1950). *Personality and language in Society*.Oxford: Oxford University Press.
- Fromkin, V.Rodman, R and Hyems (2003). *An Introduction to Language*.7<sup>th</sup> (ed) Boston: Wardswarth. Thempson Corporation.
- \_\_\_\_\_ (1988). *Introduction to Language*.Holt, Renechart and Winston.
- Fusold, R.(1994). *Socialinguistics of Language. Introduction Sociolinguistics*, Vol.11 Oxford: Blackwell.
- Githrie P. (1967). *Classification of Bantu Languages*.London Oxford University Press for the International African Institute.
- Glady, J. (1997a). *Foundation of Meanings: Primary Metaphor and Primary Scenes*. Unpublished PHD dissertation University of California, Berkely.

- Glady, W. Dobrovolsly, M. Aronoff, M. (1997). *Contemporary Linguistics*. St.Martins Press, Inc. New York. U.S.A.
- Gordon W. Norman, L. Fulton (1963). *Taboo Topics*. New York: Atherton Press.
- Guthrie, M. (1948). *Classification of Bantu Languages*. London: International African Institute Press.
- Halliday.M.A.K (1978). *Languages a Sociosemiotic.The Social Interpretation of Language and Meaning*. London: Edward Arnold and Stoughton.
- Harry, H. (1954). *Language in Culture*. Chigaco: The University of Chicago Press.
- Hudsod (1995). *Language and Society*. London: Macmillan Publishers.
- Hymes, D. (1964). *A Language, Culture and Society*. New Yolk: Herper and Row Publishers.
- Igboanusi, H. (2001). *Language Attitudes and Language Conflict in West Africa*: Enicrowfit Publishers.
- Indigas, N. (1988). *Stylistics*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Kuhenga, C. 1977). *Tamathali za Usemi*. Dar-es- salaam: East African literature Bureau.
- Marshall C. and Rossman G.B. 1999). *Designing Qualitive Research* (3<sup>rd</sup> edition) London: Sage publication.
- Mazrui, A. and Shariff, I.N. (1994). *The Swahili Idiom and Identity of an African people*. Trenton: N. J. Africa World Press.
- Mkaria, J. (2010). *Miiko na Tasfida ya Wameru, Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu Cha Nairobi.
- Mbaya M. (2002). *Linguistics Taboo in African Marriage Contex*. Astudy of the Focus Publications Ltd.

- Msokile (1993). *Msingi ya Ukakiki ya Fasihi*, Nairobi E.A.EP.
- Munyiri, J.N. (2006). *Gender and Language .A Case of the Gi- Kabete variety of Kikuyu.* M.A Thesis. Chuo Kikuu Cha Nairobi.
- Nguti, M. (2003). *Tasfida ya Kinyumbani ya Waswahili na Wakamba*. UnpublishedM.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.
- Njeri S. (2007). *A Pragmatic Analysis of Kikuyu Lexical Euphemism in HIV/AIDS Discourages*.Hakijachapishwa M.A. Thesis, University of Nairobi.
- Njogu, K. and Chimera R. (1990). *Ufundishaji wa Fasihi* .Jomo Kenyatta Foundation Nairobi.
- Peter B.(1995). *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory*. London: ManchesterUniversity Press.
- Pinker, Steven (2007). *Stuff of Thought*. London, England: Penguin Books.
- Quad-ALNasser, S. (2009). “*A Socialinguistic Comparison of Euphemisms in English and Arabic*”: Taibah University.
- Richard J. and Schmidt R. (2010). *Longhorn Dictionary of Language. Teaching and Applied Linguistic 3<sup>rd</sup> edition*.
- Spear, T.T (1978). *The Kaya Complex*, Kenya Litreture Bureau: Nairobi.
- Stock Well P. (2002). *Socialinguistic: A Resourse Book for Student*. New York: Tailor and Fransis.
- Tessar (2006). “*HIV/AIDS and African Language in Journal of African Voice*.
- Trudgill P. (2002). *Socialinguistics: An Introduction to Language and Society 4<sup>th</sup> ed.* London: Penguin books:

- Trudgill, P. (1995). *Sociolinguistics: An Introduction to Language and Society* (3<sup>rd</sup> Edition), London: Penguin Books.Tuki (1981) Kamusi ya Kiswahili, Nairobi, Oxford university press.
- TUKI (2000). *English-Kiswahili Dictionary, Second Edition*. Dar-es-salam: Institute of Kiswahili Research.
- Wafula, R.M and Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: Jomo Kenyatta foundation.
- Wambua R. (2009). *A Sociolinguistic Variation in Dialectal Use of Attitudes Towards Taboo Words and Euphemism in Kikamba*. Unpublished M.A Thesis, University of Nairobi.
- Wamitila (2002). *Uhakiki wa Fasihi*. Phoenisc Publishers Ltd. Nairobi.
- (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Uandishi*. Focus publication Ltd. Nairobi.
- (2008). *Kanzi ya Fasihi. Msingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*: Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi.
- Wardhaugh, R. (2002). *An Introduction to Socialinguistics*. (4<sup>th</sup>ed). Oxford: Black well Publishers.
- Yule G. (1996) .*Pragmatics*.UK: Oxford University Press. Oromo languu Nomadii: *Journal of African studies* 11 (2) 224-235 (polite-2)-revisit.

## **VIAMBATANISHO (I)**

### **BAADHI YA WAHOJIWA**

#### **BAADHI YA WALIOHOJI WA WASWAHILI (WAJOMVU)**

#### **MIIKO NATASIFIDA YA UKIMWI YA WASWAHILI**

#### **SALIMUMWIDADISALIMU**

Huyu alituelezea juu ya mwiko wa Ukimwi ya Waswahili

<b>Maneno ya miiko</b>	<b>Maelezo</b>
Ukimwi	Ukosefu wa kuinga mwilini
<b>Tasifida</b>	<b>Maelezo</b>
Ugonjwa wa kisasa umeme	Ugonjwa mgeni ukimwi
Aliumwa na mbuzi	Ukimwi
Ngwangwa	Ukimwi

#### **MIIKO NA TASIFIDA YA VYAKULA YA WASWAHILI**

#### **MWIDADIMWIKIFUNDA**

Alituelezea juu ya miiko ya vyakula visivyoliwa na Waswahili

<b>MIIKO</b>	<b>MAELEZO</b>
CHAKUL A	Kitu kinacholiwa na watu
<b>Tasifida</b>	<b>Maelezo</b>
Nguruwe	Nguruwe
Mfu	Mnyama aliye kufa mwenyewe
Mbwa	Yeye mwenyewe na chakula kilichotiwa katika chombo kilicho rambwa na mbwa
Kupe	Panyabuku
Kondoo	Kondoo

#### **MWIKO WA NDOA YA WASWAHILI**

Fatime Salimu alituelezea juu ya ndoa ya Waswahili.

<b>MIIKO</b>	<b>MAELEZO</b>
Ndoa	Kuleta kufunganisha watu-mke na mume.

### **MIIKO YA HEDHI YA WASWAHILI.**

Fatime Salimu alituelezea mambo ya hedhi ya Waswahili.

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Hedhi	Kuwa mwezini
	Ada ya mwanamke
	Hali ya mwanamke
<b>MIIKO YA KUNYA NA KUKOJOA YA WASWAHILI (Wajomvu)</b>	
<b>Salimu Shomari alituelezea miiko ya kunya na kukojoa ya Waswahili.</b>	
<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kunya	Kwenda haja kubwa
	Kujisaidia haja kubwa
	Kwenda chooni
<b>KUKOJOA</b>	
Kukojoa	Kuenda haja ndogo
	Kutoa maji
	Kutema mate

### **Kubaka**

#### **SALIMUMWIDADI-**

Alituelezea juu ya maneno ya tumiwa ya kuhusu kubaka.

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kubaka	Kumwingilia mwanamke kwa nguvu.
Kushika lazima	Kufanya mapenzi na mtu kwa kulazimisha

### **NGONO**

Salimu Mwidadi alituelezea juu ya maneno ya tumiwayo na Waswahili juu ya ngono.

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Ngono	Kujamiana
	Tendo la uzinifu.
	Kutangamana na mtu wako.

### **KUBALEGHE**

Kubaleghe	Kufika umri kati ya miaka tisa na kumi na miwili.
	Kuoleka



## **BAADHI YA WALIOHOJIWA WA RABAI**

### **1. Mzee Daniel-Mzee wa Kaya.**

Huyu ni mzee ambaye ana umri takribani miaka sitini. Ni mzee ambaye ana hudumu kwenye Kaya la Warabai mwenye uzoefu wa mila, utamaduni na desturi za Warabai. Alitueleza juu ya vyakula ambavyo Warabai hawaruhusiwi kuvila kulingana na mila kama vile jedwali liliivoangazia.

Mwiko/tasfida	Maelezo
Munyu achikala wagwiruwa ni pyeho	Chumvia kila mtu alishi kwa na kiharusi.
Uchiuriobumwa madzi	Tembo lililotiwa maji
Tsalakushe	Mboga mwitu
Chisonya cha miya	Mchicha wa mwitu

Vyakula hivi alituambia kwamba Warabai hawaruhusiwi kula kwa tisho kwamba watadhurika wakila.

### **2. Mgosi Mlango.**

Huyu ni mzee mwenye umri wa miaka hamsini na tano anayeishi kijijiini Uwanja wa Ndege Rabai Mpya. Alituelezea juu ya maradhi haswa majina ya tumiwayokuta ja ukimwi.

Mwiko/ tafsida	Maelezo
Walumwa ni mbuzi	Aliumwa na mbuzi.
Ukongo wa chisambi	Ugonjwa wa kisasa.
Yuna spaki	Ana spaki.
Wavyoga waya wa stima	Alikanyaga waya wa stima.
Ukongo mbaya	Ugonjwa mbaya.
Yuna mdudu	Ana mdudu.
Yuna ngoma	Ana ngoma.
Mkongo wadzenyakare	Mgonjwa wa nimekunyatayari.
Walumwa ni kabuzi	Aliumwa na kambuzi

Alituambia kwamba Warabai walitumia misemo hii ya tafsida kuashiria miiko ya Ukimwi ili kupunguza taharuki ya mwaathiriwa.

### **3. Salma Khalifani.**

Alikuwa mmoja wa wahojiwa. Ni mama wa umri wamiaka thelathini na mitano aliyetuelezea juu ya miiko ya wanyama wasioliwa na Warabai

Mwiko/Tafsida	Maelezo
Mnyama wa nyasini	Nyoka
Tsimba	Simba
Tsui	Chui
Fisi	Fisi
Ng'onzi	Kondoo
Panyabuku	Kupe
Gungu	Kunguru
Paka	Paka
Tsongo aryaye nyama	Ndege alaye nyama.

Hawa ndio wanyama aliosema hawaliwi na Warabai kwa tisho la madhara mtu afanya vyo hivyo

### **4. Mzee Mbaji Saburi.**

Ni mzee an aeishikijiji cha Ganga Rabai Mpya mwenye umri wa miaka sitini Alitueleza juu ya miiko ya kubaleghe.

Mwiko/tafsida	Maelezo
Yuvunzaungo	Amevunja ungo
Yubalehe	Amebale ghe
Yukala mtu mzima	Amekuwa mtumzima
Yuvunza umiro	Amefanya sauti nzito
Yukala mlume	Amekuwa mume
Yukala msichana	Amekuwa msichana
Yufikawa mche	Amekuwa wamke
Yufikawa kuhala	Amefika wakuoa
Yutimira	Ametimia

### **Mambo yamwili**

Mwiko	Maneno ya upole
Kunya	Hajakubwa
Kuzaa	Kugawanya maroho – kujifungua
Ngono	Kulala na mwanamke

## KIFO

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Kifo	Kuagadunia
Kwenda mbere za hachi	Kwenda mbele za haki
Kuhuricha	Kutuacha
Yuvere	Amelala
Yulumu gunia	Ameuma gunia

<b>Mwiko</b>	<b>Maelezo</b>
Ukimwi	Ukimwi
Gwangula	Ugonjwa wa ngozi
Walumwa ni mbuzi	Aliumwa na mbuzi
Yunaspacki	Ana spaki
Wavyoga waya wa spaki	Alikanyaga waya wa spaki
Ukongo wa chisambi	Ugonjwa wa kisasa
Ukongo mbya	Ugonjwa mbaya
Nidzenya kare	Nimekunya tayari

## **KIAMBATANISHO II - HOJAJI**

MIIKO NA TASFIDA YA WASWAHILI (WAJOMVU)

MIIKO NA MANENO YA UPOLE (TASFIDA)

1. Wewe huzungumza lugha gani?\_\_\_\_\_

2. Jinsia

Mke [ ]

Mme [ ]

3. Umri

Miaka 12 - 20 [ ]

Miaka 21 – 30 [ ]

Miaka 31 – 40 [ ]

Miaka 41 – 50 [ ]

Miaka 51 – 60 [ ]

4. Thibitisha kiwango chako cha elimu

CPE [ ]

KCE [ ]

KCSE [ ]

KACE [ ]

5. Sitashahada

B.A [ ]

BED [ ]

MA [ ]

6. Unaishi wapi?

Mashambani [ ]

Mjini [ ]

7. Unaelewa nini juu ya miiko? \_\_\_\_\_

Yanayokatazwa katika jamii. [ ]

Yanayokubaliwa katika jamii ya Wajomvu. [ ]

8. Maneno yafuatayo hayatajwi bure katika Kijomvu. Maneno gani ya upole

hutumiwa mbadala\_\_\_\_\_

9. Mwiko-kunya, kifo, kuzaa na kubaka. Maneno badala yake-kwenda msalani,

ametuacha, kujifungua, na kunajisi\_\_\_\_\_

10. Isimulughajamii ambapo maneno yaliyotajwayawezakutumika\_\_\_\_\_

Kunazo haliambapo maneno hayahutumika?

NDIO [ ]

LA [ ]

11. Katika mazingira gani wawezatumia maneno yaliyotajwa hapo juu

Wawezakutumia maneno haya mbele ya wanao?

NDIO [ ]

LA [ ]

Kama ndio, niyapi?\_\_\_\_\_

12. Ungetumia maneno haya ukiongea na watu wa rikalako?\_\_\_\_\_

NDIO [ ]

LA [ ]

**13.** Kama ndio ambatanisha moja ambalo halijajazwa na matano  
yaliyojazwa\_\_\_\_\_

**KIAMBATANISHO (2)**

**HOJAJI**

**MIIKO NA TAFSIDA YA WARABAI.**

**MIIKO NA MANENO YA UPOLE (TASFIDA)**

1. Wewe huzungumza lugha gani?
2. Jinsia

Mke [ ]

Mume [ ]

3. Umri

Miaka 12– 20 [ ]

Miaka 21 – 30 [ ]

Miaka 31 – 40 [ ]

Miaka 41 – 50 [ ]

Miaka 51 – 60 [ ]

4. Thibitisha kiwango chako cha elimu

CPE [ ]

KCE [ ]

KCSE [ ]

KACE [ ]

Sitashahada

B.A [ ]

BED [ ]

MA [ ]

PHD [ ]

5. Unaishi wapi?

Mashambani [ ]

Mjini [ ]

6. Unaelewa nini juu ya miiko?

A. Yanayokatazwa katika jamii.[ ]

B. YanayokabiliwakatikajamiiWarabai [ ]

7. Maneno yafuatayo hayatajwi bure katika Kirabai. Maneno gani ya upole hutumiwa mbadala.

**Mwiko**-kunya, kifo, kuzaa na kubaka. **Maneno badala yake**-kwenda msalani, ametuacha, kujifungua, na kunajisi.

(iv). Isimulugha jamii ambapo maneno yaliyotajwa yawezakutumika.

i. Kunazohali ambapo maneno haya hutumika?

NDIO [ ]

LA [ ]

ii. Katika mazingira gani wavezatumia maneno yaliyotajwa hapo juu

iii. Wavezakutumia maneno haya mbele ya wanao?

NDIO [ ]

LA [ ]

Kama ndio, ni yapi?

iv. Ungetumia maneno haya ukiongea na watu warika lako?

NDIO [ ]

LA [ ]

Kama ndio ambatanisha moja ambalo halijajazwa na matano yaliyojazwa.